
**Mkandarasi** arejesha bilioni 27/- za mradi wa maji

UKURASA 2



**Watumishi** wasimamishwa kazi madai ya kushindwa kupima COVID- 19 U/ndege

UKURASA 3





# Nipashe

Jumatano Julai 14, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580641

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# RC atofautiana na Waziri

**•NI** kuhusu muda wa zaida masomo, asisitiza kambi za mitihani kwake ni lazima... *Endelea ukurasa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akifurahia tuzo ambazo benki hiyo imezipata za "Benki Bora Tanzania" na "Benki inayoongoza kwa Ubunifu" ilizotunukiwa na Jarida la Global Finance. Waliobeba tuzo hizo ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (kushoto) na Meneja Mipango ya Biashara, Masele Msita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 3

## RC ATAJA SABABU MBILI KUZIDIWA MOTO KARIAKOO

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema miundombinu duni ya kuzima moto na mlipuko wa kemikali, ni miongoni mwa yaliyowafanya wakwame kuudhibiti moto uliolipuka katika Soko la Kariakoo Jumamosi usiku.

Makalla aliliambia BBC juzi asubuhi kwamba walifanikiwa kumudu moto kwa maji katika maduka ya chini, lakini ghafla walielemewa ulipofika ghorofani ambako zaidi ni maduka ya bidhaa za kilimo.

Mkuu wa Mkoa huyo anayeongoza Kamati ya Uchunguzi...

# Mwongozo kujikinga na corona wapuuzwa

UKURASA 2

## Suruali yatengua kifungo miaka 30

UKURASA 3

**MICHEZO** **GOMES AFUNGUKA WATACHEKA KIGOMA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# RC atofautiana na Wizara ya Elimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameonyesha kutofautiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu muda wa masomo na kambi kwa ajili ya madarasa ya wanafunzi wanaojiandaa kufanya mitihani ya taifa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wananchi wa Kata ya Makulu jijini hapa ikiwa ni sehemu ya kampeni yake ya kutatua migogoro ya ardhi, Mtaka alisema katika suala la elimu, ni vyema wananchi wakasikiliza viongozi wa mkoa na kuomba wazazi wawaruhusu watoto wa madarasa hayo kufanya kambi za kitaaluma.

Alisema suala la elimu kwake ni kipaumbele na hahitaji ushauri wa mwanasiasa kwenye jambo hilo kwa kuwa Dodoma ni ya mwisho katika matokeo ya mitihani ya darasa la nne, saba na vidato vya pili na nne.

"Watoto waende shule, nimeanza kuwaambia wazazi waruhusu watoto kuanza kambi za maandalizi ya mtihani ya taifa, msisikilize ushauri wa watu wanaowaambia kambi zisiwapo, hao wanaowaambia watoto wao wanasoma shule za ada Sh. milioni 10, hawasomi shule za kata.

"Maana yangu ni kwamba msisikilize ushauri wa waziri anayekwambia kusiwapo na kambi, muulize 'kwani mwenzetu watoto wako wanasoma wapi?' wenzako watoto wao wanasoma Canada, hawajui shule ya kata kama hakuna mwalimu wa Fizikia wala Kemia," alisema.

Mtaka alisema suala la watoto kusoma kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa na nusu jioni kwa kisingizio ndiyo mwongozo wa serikali, halisaidii kuongeza ufaulu kwenye mkoa huo.

"Anakwambia mtoto mwisho kusoma saa tisa, mimi ninawafahamu watoto kwa sababu wanashinda barabarani, kwenye suala la elimu nisikilizeni mimi ninayekaa na watoto kwenye kata.

"Watoto waingie kambini, kama wanaanza saa moja kusoma wanaanza kusoma, huyo waziri anayekushauri, watoto wake wanasoma international school (shule ya kimataifa), kama watoto wanasoma hadi saa 11 jioni ina maana shule na wazazi wamekubaliana," alisema.

Alitoa wito kwa wazazi na uongozi wa shule kukubaliana namna nzuri ya kuwasaidia watoto kufanya maandalizi ya ziada kwa ajili ya mitihani.

"Anayekwambia watoto wasome hadi saa tisa na nusu, watoto wake wanasoma tuition (masomo ya ziada) nyumbani, wanapelekwa na gari la bendera, wanarudishwa na gari la bendera nyumbani na mwalimu anawafuata watoto nyumbani kuwafundisha.

"Akitoka kwenye TV anasema mwisho wa watoto kufundishwa ni saa tisa, anasubiri atangaze watoto wako wamepata sifuri na division four (daraja la nne) kwenye matokeo."

Alisema anataka vyuo vilivyopo Dodoma, vijae wanafunzi wa Dodoma na wananchi wawe na uchungu wa kusimamia suala la elimu.

"Kwenye suala la elimu mnisikilize mimi ambaye nipo na ninyi kwenye kata, msije mkasikiliza mtu ambaye yupo kwenye kiyoyozi...

"Watoto wake wanasoma nje, international school, aje akuelekeze wewe mzazi unayesomesha mtoto kwenye shule ya elimu bure ya Mama Samia," alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema mzazi mwenye mtoto wa darasa la saba na kidato cha nne, akae na uongozi wa shule wakubaliane ili watoto wao wafanye vizuri kwenye mitihani.

"Wapo wazazi leo wako tayari kuchagua hata walimu ambao hawapo kwenye shule wasaidie watoto, na ndiyo maana unamsikia mtu watoto wasome hadi saa tisa, halafu anakwambia tena kuna shule watoto hawajawahi kumuona mwalimu wa Fizikia na Baiolojia.

"Mwenzako anakuja kwenye shule kukagua darasa limejengwa, hajui mtoto anatembea kilometa 10 kwa siku kusoma, mtu wa aina hiyo mpuuze, ninasisitiza kwenye suala la elimu wasikilizeni viongozi wa mkoa tunaokaa na watoto wetu kwenye shule za kata.

"Usimsikilize mtu kwa sababu ya uwaziri, hajui watoto wanatembea kilomita 50 kwa wiki," alisema.

Alitoa wito kwa wazazi wote wenye watoto wa darasa la saba na kidato cha nne wakae na uongozi wa shule husika wakubaliane.

"Hawa watoto wamekaa UMISETA mwezi mzima, walikuwa wanalala wapi? Walikuwa wanalala kwenye madarasa hayo, wamelala madarasani kucheza UMISHUMTA, UMISETA, wakilala kusoma ni dhambi?

"Mtu anayesema hivyo, unamsikiliza unamwombea kwa Mungu, simamieni watoto wasome, ili wazawa wa Dodoma muwe washindani," aliagiza.

Mkuu wa Mkoa huyo alionya kuwa watoto wao wasiposoma, watakuwa vibarua wa Makao Makuu.

"Yatajengwa maghorofa, vitajengwa viwanda, mtauza mashamba, mtoto kibarua, kitukuu kibarua, kirembwe kibarua, ukoo wa vibarua wa Makao Makuu.

"Msikubali huo ujinga, bebeni uchungu wa watoto wa Dodoma kusoma, siwezi kukubali, watoto wa Dodoma wana akili, subirini waingie kambini kama hawajapata division one (daraja la kwanza," alitamba.

Alisisitiza kuwa wapo wakazi wa mkoa huo wamedhulumiwa ardhi kutokana na kukosa elimu.

"Haya maneno makavu makavu ninawaambia mpate hasira ya kusomesha, mbona hawajamdhulumu Mzee Malecela, Ndugai, Kusila, wanakudhulumu wewe ambaye cheti cha darasa la saba kwako hakipo, pa kwenda huna, unabaki unamlilia Mungu, someshени watoto.

"Mkisoma hakuna mtu atakayechukua viwanja 10 anakupa vitatu kwenye makorongo, huu ujinga mtaukataa kwa kusomesha watoto," alisema.

Hivi karibuni, Wizara ya Elimu kupitia kwa waziri wake, Profesa Ndalichako, ilionya kuhusu shule kuwa na vipindi vingi kwa wanafunzi, vinavyofanyika nje ya muda uliowekwa na wizara.

Katika ukurasa wake wa Facebook, jana Mkuu huyo wa Mkoa aliomba radhi kwa tafsiri iliyojitokeza kwenye ujumbe wake hasa alipotolea mfano wa Waziri.

Aliandika "Nimesoma na kupokea maoni, ushauri na kila aina ya hisia ambazo naamini ni kwa upendo juu ya 'clip' yangu kuhusu kambi za kitaaluma nilipokuwa nikizungumza na wananchi wetu katika tafsiri yoyote ile naomba radhi kwa wote waliokwazika, wananchi na viongozi wenzangu hasa pale matumizi ya neno 'Waziri' lilipobeba hisia tofauti, nawaheshimu mawaziri wote na nafanya nao kazi kwa ushirikiano mkubwa."

"Natambua kazi nzuri inayofanywa na mawaziri wetu wanaosimamia sekta ya elimu. Wapo wanaodhani maelezo ya hisia zangu ni kuanza kupandisha mabega, na pengine mgema akisifiwa tembo hutia maji - niwaondoe hofu sina sababu ya kupandisha mabega," alisisitiza.

# Mkandarasi kurejesha bil. 27/-

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Maji amesema Sh. bilioni 27 za mradi wa maji wa Mwanga -Same-Korogwe alizokuwa amelipwa mkandarasi wa mradi huo, zitarejeshwa baada ya kubainika kuwapo udanganyifu.

Jumaa Awesso aliyasema hayo juzi jioni alipozungumza na viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema mbali na hilo, ameitaka Wizara ya Maji kuhakikisha ndani ya siku tatu inawalipa watumishi wote waliokuwa wakidai fedha zao katika mradi pamoja na mafao ya NSSF yapatayo Sh. milioni 913.7.

Awesso alisema mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na vikwazo vya makandarasi, hali iliyosababisha serikali kusitisha mikataba yao.

Awesso alisema mkandarasi huyo ambaye ni Badr East Africa Enterprises Ltd, anadaiwa kufanya udanganyifu katika nyaraka zilizosababisha kulipwa kiasi hicho cha fedha.

Alifafanua kwamba baada ya kuhojiwa na vyombo vya dola, mkandarasi huyo alikiri kugushi nyaraka hizo na kuahidi kurejesha fedha.

Alibainisha kwamba kwa sasa wizara kupitia kwa wataalamu wake wa ndani wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) wanaendelea na baadhi ya shughuli katika mradi huo ikiwamo ufungaji wa mabomba kutoka Kisangara-Kiverenge -Vudoi yenye urefu wa kilomita 70 ambapo mpaka sasa wamefunga kilomita 44.

Aliwataka wataalamu wa maji katika mradi huo kuacha tabia ya kuhujumu mradi huo, akitolea mfano eneo la Kisangara lililoandikiwa ripoti ya kuhitajika kufungwa pampu za kuvutia maji 11 wakati uhalisia zinahitajika pampu sita.

Waziri huyo aliongeza kuwa katika bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/22, serikali imetenga Sh. bilioni 19 kwa Mkoa wa Kilimanjaro kwenda kumaliza matatizo ya maji.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Anthony Sanga, alisema mradi wa maji Same-Mwanga-Korogwe ni miongoni mwa miradi mikubwa nchini unaogharimu Sh. bilioni 262, ukitarajiwa kuhudumia wananchi 438,820.

# Mwongozo kujikinga na corona wapuuzwa

**Na Romana Mallya**

TAHADHARI na mwongozo wa kitaifa kukabili corona ni kama umepuuzwa katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na kinachoshuhudiwa sasa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo wa kibiashara ikiwamo kwenye masoko na hata usafiri pendwa wa daladala.

Ufuatiliaji wa Nipashe kuhusu utekelezaji wa mwongozo huo ambao pamoja na mambo mengine, unazuia msongamano wa watu na kuhimiza uvaaji wa barakoa, umebaini kutozingatiwa kwa utaratibu huo.

Katika masoko mbalimbali ambayo Nipashe imeyafikia, likiwamo Soko la Kariakoo ambalo kwa siku limekuwa likipokea maelfu ya watu wakiwamo kutoka nchi jirani, mwongozo wa afya dhidi ya corona umepuuzwa na wananchi wanaendelea na maisha kama kawaida.

Tahadhari ambazo serikali imekuwa ikizitoa tangu Machi mwaka jana ugonjwa huo ulipoingia Tanzania na inaendelea kuzisisitiza hadi sasa, kwa kiwango kikubwa hazizingatiwi.

Licha ya mkoa huo kuwa na idadi kubwa ya watu inayosababisha msongamano, Nipashe imeshuhudia katika maeneo mbalimbali hakuna vifaa vya kunawia mikono ambavyo mwaka jana vilitakiwa kuwekwa kila eneo la kutoa huduma.

Mbali ya masoko, katika usafiri wa umma ambapo miongoni mwa maelekezo ni kuhakikisha wanabeba abiria kwa idadi ya viti, Nipashe imeshuhudia vyombo hivyo vikibeba kwa kuwajaza na miongoni mwao waliovaa barakoa, ni wachache na wakati mwingine asiwapo hata mmoja aliyevaa.

Mmoja wa abiria ambaye alikutwa kwenye daladala linaloelekea Soko la Kariakoo, Joseph George, alipoulizwa sababu za kutozingatia mwongozo wa serikali, ikiwamo kutovaa barakoa, alisema hata akivaa kama ameandikiwa kufa, atakufa tu.

Mwajuma Ally, aliyekutwa na Nipashe kwenye Soko la Kariakoo juzi, akiendelea na ununuzi wa bidhaa huku akiwa amevaa barakoa, alisema hawezi kuacha kuvaa kwa sababu tayari serikali imeshatangaza Tanzania kuna corona.

Aliitaka serikali iendelee kutoa elimu zaidi ikiwezekana kwa magari ya matangazo hasa kwenye mikusanyiko ili wananchi ambao bado wanaona hakuna corona, wajue ipo.

**HABARI KITAIFA**

# Suruali yatengua kifungo miaka 30

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Shinyanga imeamwachia huru Daudi Manamba aliyekuwa anatumikia kifungo cha miaka 30 jela baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumwingilia kinyume cha maumbile mwanafunzi wa miaka sita.

Mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu, mahakama ilitoa uamuzi huo baada ya kusikiliza rufani iliyokatwa na Manamba akipinga adhabu aliyopewa ya miaka 30 jela na Mahakama ya Wilaya ya Kahama.

Mrufani alipinga adhabu kwa madai kwamba Upande wa Jamhuri hakuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka.

Upande wa Jamhuri ukiwakilishwa na Wakili wa Serikali, Enosh Kigoryo, ulidai Jamhuri imethibitisha bila kuacha shaka katika ushahidi wa mashahidi watatu akiwamo baba wa mtoto aliyebakwa.

Ulidai ushahidi unaonyesha tukio lilitokea Januari 21, mwaka 2017, maeneo ya Zongomela wilayani Kahama, baba wa mtoto akidai aliona damu katika suruali ya mtoto na alipomuuliza, alimtaja mrufani kuwa alimbaka.

Inadaiwa mtoto alikuwa akitoka shuleni, akiwa njiani alikutana na mrufani, akampeleka kwenye majani, akamwelekeza ainame, alimvua suruali na kuanza kumwingilia huku akiwa amemziba mdomo na kumtishia kumuua endapo angesema kwa mtu yeyote. Alidai mtoto alikuwa akilia, lakini mrufani alimziba mdomo na kumtishia, ripoti ya daktari na ushahidi wa uchunguzi ulionyesha alibakwa na sehemu yake ya nyuma ilikuwa wazi kiasi ambacho kitu chochote kinaweza kupita.

Mahakama ya Wilaya iliona mashtaka yamethibitika bila kuacha shaka, hivyo mrufani alitiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela miaka 30.

Mrufani alipinga adhabu hiyo kwa madai kwamba mashtaka dhidi yake hayakuthibitika.

Mahakama baada ya kusikiliza rufani hiyo, iliikubali hoja za aliyekata rufani kwa kuwa katika ushahidi, ni vigumu kujua tukio lilitokea maeneo gani.

Sababu ya pili, suruali iliyokuwa ikidaiwa kuwa na damu haikutolewa mahakamani kama kielelezo na ushahidi wa upande wa mashtaka haukuwa na nguvu za kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka.

"Kwa kusema hayo, rufani inakubaliwa, adhabu ya miaka 30 jela inafutwa na mahakama inaamuru mrufani aachiwe huru gerezani," alisema Jaji Mkwizu.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jana. **PICHA: IKULU**

# Watumishi wasimamishwa madai ya kushindwa kupima COVID- 19 U/ndege

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Abel Makubi, amewasimamisha kazi watumishi tisa wa kitengo cha upimaji wa virusi vya corona katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Peof. Makubi alitoa agizo hilo juzi usiku jijini Dar es Salaam alipofanya ziara uwanjani huko kukagua utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa.

Alitaja sababu za kuwasimamisha kazi kuwa ni utovu wa nidhamu uliofanywa na watumishi hao kwa kutokufika kazini bila kutoa taarifa rasmi kwa uongozi.

"Jana (juzi), watumishi wanane hawakufika kazini na leo (jana) mmoja bila kutoa sababu ya msingi, jumla wanakuwa tisa," alisema Profesa Makubi.

Alisema utaratibu huo unaonyesha kuwa baadhi ya watumishi kutokwenda kazini ni jambo la kawaida na viongozi wamekuwa hawachukui hatua zozote.

"Kwa hiyo, hawa ambao hawakufika jana (juzi) jumla walikuwa wanane na kati yao wanne walikuwa wameajiriwa na Wizara ya Afya na wanne wameajiriwa na Manispaa ya Dar es Salaam, wapo chini ya RAS wa Dar es Salaam. Nimeagiza hawa walio chini ya Wizara ya Afya wasimame kufanya kazi ili tufanye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki," alisisitiza Profesa Makubi.

Alishauri waliojiriwa na Ofisi ya RAS wachukuliwe hatua stahiki na mamlaka zao kama zilizochukuliwa na Wizara ya Afya.

Prof. Makubi alisema pia wanafanya utaratibu wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi na watumishi hao tisa ili kazi iendelee.

Aliwataka watumishi wote wa Sekta ya Afya kutanguliza uzalendo katika utendaji wa kazi zao na kwa kujituma.

"Hapa tunapofanya upimaji ni upimaji unawakilisha sura ya nchi yetu. Kwa hiyo, mtu yeyote anayeletwa hapa maana yake ndiye anayetoa taswira ya nchi yetu kwa ujumla," alisema Profesa Makubi.

Alisema maelekezo waliyoyatoa ya kuongeza watumishi 20 katika eneo la upimaji wa corona yametekelezwa.

"Nimefarijika kuna maboresho zaidi yamefanyika, hasa hasa kuongeza sehemu za kupima lakini maeneo ambayo abiria wanaweza kuwa wanapimwa.

"Nimeona wameongeza upande mmoja ambao abiria watakuwa wanaingia wakifuata mstari na pia kwa umbali wa mita moja moja kwa kuachana," alisifu.

Alisema wamechukua hatua hizo kutokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria katika uwanja huo.

# RC ataja sababu mbili kuzidiwa moto Kariakoo

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema miundombinu duni ya kuzima moto na mlipuko wa kemikali, ni miongoni mwa yaliyowafanya wakwame kudhibiti moto uliolipuka katika Soko la Kariakoo Jumamosi usiku.

Makalla aliliambia BBC juzi asubuhi kwamba walifanikiwa kumudu moto kwa maji katika maduka ya chini, lakini ghafla walielemewa ulipofika ghorofani ambako zaidi ni maduka ya bidhaa za kilimo.

Mkuu wa Mkoa huyo anayeongoza Kamati ya Uchunguzi iliyoundwa, pia kujitambulisha kuwa mstari wa mbele kuukabili, alisema moto uliingia ghorofani wastani wa saa saba kutokana na kuwapo bidhaa za kemikali, ikiwamo aina ya Sulphur, zilizozidisha moto.

Alisema ni hali iliyowaelemea wakati huo kwa sababu hawakuwa na nyenzo za kuwafikisha kukabili moto kutoka juu na tayari ulishaongezeka maradufu, ingawa yalikuwapo maji ya kutosha.

Makalla alisema maji yalipomwagwa kwenye moto wa ghorofani hayakusaidia kutokana na uhalisia wa bidhaa zilizokuwapo katika maduka ya juu na wakati huohuo, hawakuwa na mbadala wa maji kudhibiti aina hiyo ya moto.

Alisema kikosi cha Zimamoto mara moja kilichukua mbadala wa kudhbiti moto kusambaa katika maeneo jirani na walifanikiwa, ikiwamo kutofikia soko dogo la vyakula, maduka na makazi ya watu.

Kwa mujibu Mkuu wa Mkoa, eneo la tatu la Soko la Shimoni ambako kuna wateja wengi, halikuathirika kutokana na moto, Nipashe ilishuhudia jana mitaa jirani ikiwa chini ya udhibiti na eneo lote la soko na mitaa jirani iliyozungushwa kamba ilikuwa chini ya udhibiti.

Hiyo inajumuisha sehemu ya mtaa maarufu wa biashara wa Tanandamti, eneo la Posta ya Kariakoo na maduka maarufu, kama vile la vitabu Tahfif, yalikuwa yamefungwa na eneo lilikuwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi.

Wajasirimali wanaojaa hasa katika eneo la soko dogo, walijaa katika mitaa jirani hasa unaopakana na soko dogo.

## TANGAZO

# TPB BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### TPB BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI, 2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30/06/2021 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31/03/2021 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 42,425 | 35,455 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 67,804 | 11,378 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 115,988 | 89,590 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 88,611 | 76,304 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (35) | 727 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 133,356 | 81,030 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 658,761 | 654,724 |
| 12 | Mali Nyingine | 46,141 | 45,245 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 23,332 | 22,840 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,176,384** | **1,017,295** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 754,781 | 668,094 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 212,906 | 99,385 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 5,730 | 9,038 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | 2 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 20,996 | 21,965 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 2,254 | 2,391 |
| 27 | Dhima Nyingine | 28,567 | 30,682 |
| 28 | Madeni | 40,920 | 78,873 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,066,155** | **910,430** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **110,229** | **106,864** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 66,533 | 66,533 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 7,534 | 2,566 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 8,090 | 9,694 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **110,229** | **106,864** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 0 | 0 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 82,434 | 96,813 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 21,900 | 20,215 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 27 | 40 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.37% | 10.50% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 12.00% | 14.26% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 91.00% | 101.60% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 56.00% | 64.36% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 73.29% | 80.76% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 12.98% | 0.39% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 15.64% | -2.53% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | Robo ya Mwaka sasa 30/06/2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30/06/2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/06/2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30/06/2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 33,297 | 29,848 | 65,355 | 54,257 |
| 2 Gharama za Riba | (9,716) | (8,509) | (19,246) | (16,021) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **23,580** | **21,339** | **46,110** | **38,236** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 1,533 | (103) | (85) | (322) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,393) | (2,100) | (6,941) | (4,535) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **9,622** | **5,370** | **18,512** | **14,411** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 1,428 | 1,283 | 2,587 | 1,942 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,150 | 1,855 | 8,714 | 6,648 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 4,044 | 2,232 | 7,211 | 5,821 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(23,823)** | **(19,031)** | **(45,560)** | **(35,845)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 11,216 | 9,209 | 22,458 | 17,432 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1,235 | 1,683 | 2,422 | 2,480 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 11,372 | 8,139 | 20,679 | 15,934 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **7,520** | **5,476** | **12,036** | **11,945** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 2,552 | 1,774 | 4,502 | 3,549 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **4,968** | **3,702** | **7,534** | **8,396** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **4,968** | **3,702** | **7,534** | **8,396** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,060 | 1,057 | 1,060 | 1,057 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 177 | 132 | 268 | 299 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 42 | 43 | 42 | 43 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.44% | 0.47% | 0.89% | 1.15% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.59% | 3.34% | 7.02% | 7.92% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 55.51% | 54.04% | 54.32% | 52.20% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.73% | 3.22% | 5.48% | 6.31% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI, 2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi Mwaka wa uliopita 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 7,520 | 4,516 | 12,036 | 11,945 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 4,151 | 7,450 | 11,601 | 11,347 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (4,037) | (36,911) | (40,948) | (182,624) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 200,207 | (24,437) | 175,770 | 272,819 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (21,004) | (1,267) | (25,290) | 65,114 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (29,896) | (3,425) | (30,679) | (34,996) |
| - Kodi Iliyolipwa | (2,552) | (1,950) | (4,502) | (3,549) |
| - Mengineyo (bainisha) | (29,015) | (9,947) | (38,587) | (128,685) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | 125,374 | (65,972) | 59,402 | 11,371 |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,872) | (1,591) | (3,463) | (1,109) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | (1,872) | (1,591) | (3,463) | (1,109) |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (1,226) | (1,513) | (2,738) | (3,405) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | *(1,226)* | *(1,513)* | *(2,738)* | *(3,405)* |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 122,276 | (69,075) | 53,201 | 6,857 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **51,451** | **120,526** | **120,526** | **17,102** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 173,727 | 51,451 | 173,727 | 23,959 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | **7,534** | **7,534** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | **(1,604)** | **(1,604)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | - | - | - | - | - | - | **110,229** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | **(0)** | **0** | **10,220** | **98,893** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 5,866 | - | - | - | **5,866** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 66 | - | - | - | **66** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | (526) | **(526)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI, 2021**

Benki ililipa faini ya shilingi 1,000,000 kwa kuchewa kupeleka taarifa ya ukwasi Benki Kuu.

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | **IMESAINIWA** | **13.07.2021** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | **IMESAINIWA** | **13.07.2021** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | **IMESAINIWA** | **13.07.2021** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa **zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi**

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | **IMESAINIWA** | **13.07.2021** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI** Mjumbe wa Bodi | **IMESAINIWA** | **13.07.2021** |

Head Office: LAPF Towers Bagamoyo Roard. P.O. Box 9300 Dar es Salaam Tanzania. Telephone: +255 22 2162940, Fax: +255 22 2114815, Email: info@tpbbank.co.tz

## TANGAZO

Tpb Bank
Grow with us

# TPB BANK TARIFF GUIDE 2021

| BANK CHARGES | | |
|---|---|---|
| ITEM | FEE DESCRIPTION | TZS |
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Tabasamu Individual | 10,000 |
| | Tabasamu Group Account | 50,000 |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Group Account | FREE |
| | Scout Minor Account | 10,000 |
| | Scout Account | 30,000 |
| | Yanga VIP Account | 1,200,000 |
| | Yanga Members Account | 25,000 |
| | Wavuvi Account | 10,000 |
| | Current / Call Account | 100,000 |
| | Fixed Deposit Account | 100,000 |
| | WADU Account | 20,000 |

| MAINTENANCE FEE | FEE DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Personal Call Account | Per Month | 6,500 |
| Corporate Call Account | Per Month | 10,000 |
| **Savings Accounts** | | |
| Quick Account | Per Month | 1,560 |
| Salary Account | Per Month | 1,560 |
| Tabasamu Individual / Group Account | Per Month | FREE |
| Platinum Account | Per Month | 1,560 |
| WADU Account | Per Month | FREE |
| Minor Account | Per Month | FREE |
| Group Account | Per Month | FREE |
| Scout Junior Account | Per Month | FREE |
| Scout Senior Account | Per Month | FREE |
| Yanga VIP/ Members Account | | 1,560 |
| Yanga Members Account | | 1,560 |
| Wavuvi Account | | 1,560 |
| **Cash Deposit** | | |
| Over the Counter | Per Transaction | FREE |
| Popote Agents | Per Transaction | FREE |
| **Bank Statement** | Per Page | 2,000 |

| CASH WITHDRAWAL OVER THE COUNTER | | |
|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | TZS |
| All Accounts | Teller Withdraw up to 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller Withdraw form 10,000,000 - 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller Withdraw form 50,000,001 - 100,000,000 | 15,000 |
| | TellerWithdraw above 100,000,001 | 30,000 |

| ATM CASH WITHDRAW | | |
|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | TZS |
| TPB Bank ATMs | Per Transaction | 1,300 |
| Other Banks Umoja Switch ATMs | Per Transaction | 1,300 |

| OTHER ATM & NORMAL CARDS FEE | |
|---|---|
| TRANSACTION / ITEM | TZS |
| PIN Re - Issue | FREE |
| Collection of ATM Card at Non Domicile Branch | 6,500 |
| Uncollected and destroyed ATM Card | 6,500 |
| First ID Card ( Local and Foreign Currency ) | 4,000 |
| Replacement of ID Card | 2,600 |

| BANK CHARGES | | |
|---|---|---|
| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
| Cheque Book | Per Leaf | 500 Per leaf or equivalent in foreign currency |
| Cheque Clearing Fee | Per Cheque | FREE |
| Unpaid Cheques / Insufficient Funds | Per Cheque | 150,000 TZS And Equivalent in Foreign Currency |
| Stop Payment Order | Per Cheque | 30,000 TZS per leaf Max. 300,000/= and Equivalent in Foreign currency. |
| **Balance Enquiry** | | |
| Over the Counter | Per Enquiry | 300 |
| At the ATMs | Per Enquiry | 300 |
| At POS Branches | Per Enquiry | 150 |
| At Popote Agents | Per Enquiry | 100 |
| At TPB Popote Mobile Banking | Per Enquiry | 300 |
| Internet Banking | Per Enquiry | FREE |

| ATM Issuance & Replacement | | |
|---|---|---|
| Popote Card | Per Card | 15,000 |
| Yanga Card | Per Card | 20,000 |
| **TRANSACTION** | **DESCRIPTION** | **TZS** |
| **Dormant Accounts** | | |
| Activations | Per Activation | FREE |
| Dormant Account Fees | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 year to 10 years | 5,000 |
| | 11 year to 15 years | 10,000 |
| **Closing of Account** | | |
| All Accounts | Per Account | 13,000 or Equiv. in Foreign Currency |
| **Funds Transfer** | | |
| Within TPB Bank Over the counter | Per Transaction | FREE |
| TPB Popote Mobile Banking | 0.01 - 10,000 | 1,000 |
| | 10,000.01 - 30,000 | 1,300 |
| | 30,000.01 - 100,000 | 2,000 |
| | 100,000.01 - 200,000 | 3,500 |
| | 200,000.01 - 500,000 | 4,500 |
| | 500,000.01 - 750,000 | 7,500 |
| | 750,000.01 - 1,000,000 | 10,000 |
| From MNOs to Bank (Deposit) | | FREE |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Internet Banking Registration | Per Registration | FREE |
| TPB Popote Mobile Banking Registration | Per Transaction | FREE |
| | **FEES** | |
| **TRANSACTION** | **DESCRIPTION** | **TZS** |
| Transfers | TISS - Outward | 10,000 TZS |
| | EFT - Outward | 2,000 TZS |
| | EFT - In House | 1,500 TZS |
| Standing Order | Within the Bank | FREE |
| | To other Banks | 13,000 TZS |
| Other Transfers | Internal Transfer | FREE |
| Others | Salary Handling - Cheque list | 1,000 TZS |
| | Introduction letter to Embassy, etc | FREE |

| LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES | | |
|---|---|---|
| LOANS | CATEGORY | INTEREST RATE |
| Consumer Loans | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved loan. Minimum TZS. 10,000/= |
| Wastaafu Loans | Loan Application fee | TZS 10,000/= |
| | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |
| Other Charges On Individual Micro Credit | MIC Loan Application fee | TZS 25,000/= |
| | MIC Loan Processing/ Administration fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |
| Interest Rates And Charges On Business Loan | Loan Application fee for Business and Personal loans | TZS. 50,000/= |
| | Loan Administration fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount. |

| USD TRANSACTION FEES | | |
|---|---|---|
| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES IN USD |
| Maintenance Fee | Savings Account | 1 |
| | Call Account | 5 |
| Deposit Fee | Non Account Holder | FREE |
| Opening Balance | | 50 |
| Bank Statement | | FREE |
| Bank Statement | Balance Enquiry - Banking Hall | FREE |
| | Confirmation letter | FREE |
| Withdraw fees | Below 50 | 1 |
| | 51 - 1,000 | 2.5 |
| | 1,000 - 2,250 | 5 |
| | 2,251 - 5,000 | 15 |
| | Above 5,000 | 0.25 Percent |
| Dormant | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re - Activation | FREE |
| TISS | | 10 |

216357502

**Head Office:** 10th Floor - LAPF Towers, Bagamoyo Road, Kijitonyama, P.O Box 9300, Dar es Salaam. **Telephone:** +255 22 2162940, **Email:** info@tpbbank.co.tz, **Website:** www.tpbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Moto wa Kariakoo umetuachia funzo

**JUMAMOSI** soko la kihistoria la Kariakoo liliteketea moto katika mazingira yenye utata, huku Jeshi la Zimamoto na Uokoaji likishindwa kukabili moto huo, kutokana na sababu nyingi zilizoelezwa, ikiwamo kukosekana kwa miundombinu ya maji na maji katika eneo hilo.

Hasara iliyopatikana ni kubwa katika soko hilo ambalo bado lilikuwa na madeni makubwa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na mwanahisa mmoja ambaye ni Jiji la Dar es Salaam, huku ikiwa zimepita siku chache tangu Rais Samia Suluhu Hassan, atembelee na kuwasimamisha kazi viongozi wa soko na kuunda tume ya uchunguzi.

Moto huo ulizuka majira ya saa 2 usiku na ilishindikana kuukabili, kutokana na kukosekana kwa maji ya kuzima, wakati makao makuu ya Zimamoto yakiwa ni Upanga, umbali wa kilomita moja.

Ni jambo la kushangaza kwamba katika eneo la Kariakoo sokoni na kwenye mitaa yenye maduka ya bidhaa za kila aina ambazo huleta wafanyabiashara kutoka nchi za Zimbabwe, Uganda, Malawi na Zambia na DRC, kwa kutaja baadhi kuna majengo mengi ya ghorofa ambayo mwonekano wake ukiwa angani ni kivutio tosha kinachopendezesha Jiji, hakuna miundombinu ya maji ya kuwezesha kujaza gari la zimamoto!

Inaelezwa walilazimika kwenda umbali mrefu kutafuta maji ya kujaza kwenye magari ndipo wauzime, jambo ambalo siyo sahihi kwa kuwa kuwa sehemu kubwa ya kodi kwenye biashara inakusanywa kutoka Kariakoo.

Kingine ni vifaa vya kupanda kwenye jengo hilo kuwa tatizo, jambo linaloonyesha wanapaswa kufanya kazi ya ziada ya namna ya kukabili matukio hayo.

Huu ni ujumbe tosha kwa serikali kwamba inatakiwa kujipanga upya hasa kwa kuwa na miundombinu ya maji katika maeneo yote muhimu, na kujiandaa kwa ajili ya kukabiliana na majanga kama hili h na mengine.

Leo tunazungumza hasara kubwa iliyowapata wafanyabiashara zaidi ya 1,662, huku waliokuwa wanalipa pango wakiwa ni 224, ambao kila mmoja mtaji wake umeteketea na sasa wamerudi sifuri, kama walikuwa wamekopa benki maana yake watashindwa kurudisha.

Lakini wamiliki wa biashara hizo hawakuwa wanafanya wenyewe bali waliajiri Watanzania wengine, ambao walijipatia kipato na kuchangia uchumi wa nchi, na sasa wanashindwa kupata kipato chochote kutokana na hasara hiyo.


Pia, wamiliki na waliokuwa wameajiriwa wana wategemezi kwa maana ya watoto wa kusomesha au wanatakiwa kulipa kodi ya nyumba, kugharamia matibabu yao na ndugu wengine. Na huenda asilimia kubwa hawakuwa wamekata bima ya biashara zao na sasa wanarudi nyuma kimaisha, hii siyo hali njema kwao binafsi na uchumi kwa ujumla.

Kushindwa kudhibiti matukio ya moto imekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wanaokumbwa na majanga hayo, kwa kuwa ni kawaida kwa gari la zimamoto kufika bila maji au kufika eneo la tukio na kuondoka kwenda kuyatafuta mbali.

Ni muhimu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakajifunza na kubadilika ili kukabili matukio ya moto kwa kuhakikisha magari yana maji na wanatumia mbinu zote kufanyakazi kwa ubora, vinginevyo watu wanapoteza imani na uwezo wao wa kukabili majanga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni kudai Katiba mpya na kujipanga 2025



Na Sabato Kasika

**MOJA** ya mambo ambayo ni ya kwanza kwa wanasiasa na wanaharakati kuyaomba kwa Rais Samia Suluhu Hassan, mara tu alipoingia madarakani, ni kukamilisha mchakato wa kupata Katiba mpya.

Pamoja na madai hayo, ipo haja ya kuwakumbusha wanasiasa kwamba, Katiba mpya ije lakini wajipange kiuchaguzi. Ni kwa sababu mwisho wa uchaguzi huwa ni mwanzo wa maandalizi ya mwingine, kwani miaka mitano si mingi katika kujipanga.

Sasa ni miezi tisa tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28 mwaka jana, huku CCM ikiibuka na ushindi kuanzia kwenye udiwani, ubunge hadi urais. Kwa kuwa kumalizika kwa uchaguzi, huwa mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi mwingine, ingependeza kama vyama vya siasa vingejipanga ili kushiriki vyema katika uchaguzi mkuu wa 2025.

Maandalizi hayo ni pamoja na kuongeza wanachama wapya, kwa kujikita zaidi kwenye mashina na matawi ambako ndiko wananchi waliko, ili kuondoa dhana iliyojengeka kuwa vyama vya upinzani ni vya msimu.

Katiba mpya ni muhimu, lakini vyama kujiimarisha kuanzia ngazi ya chini ni jambo muhimu zaidi, kuliko kusubiri kuibuka wakati wa uchaguzi tu bila kuwa na wanachama wa kutosha wa kuviunga mkono.

Vyama kusubiri uchaguzi ni sawa na kusindikiza lakini vikiwa na wanachama wa kutosha, inakuwa ni rahisi kufurukuta na hata kufanikiwa kupata viti vya udiwani na ubunge.

Hivyo, wakati vikidai katiba, visisahau kujipanga vizuri kuanzia ngazi ya chini, kwani kufanya mikutano ya ndani kama ambavyo serikali inaelekeza, badala ya kubaki kudai katiba muda wote wakati havina wanachama wa kutosha.

Kwa maana nyingine, joto la kudai katiba mpya lisivifanye vyama vya siasa kuishia hapo, bali vipige hatua zaidi kwa kuendelea kujipanga zaidi ikiwa ni pamoja na 'kuvuna' wanachama wapya.

Uchaguzi mkuu hufanyika kila baada ya miaka mitano, na maandalizi ya uchaguzi mwingine hutakiwa kuanza, vinginevyo vyama vya upianzani vinaweza kuendelea kusindikiza chama tawala.

Ikumbukwe kwamba, tangu uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1995, baadhi ya vyama vilivyokuwa na nguvu wakati huo, vimeendelea kuyumba na vingine kushindwa kushiriki kwenye uchaguzi mkuu.

Inawezekana sababu mojawapo ya kuwapo kwa hali hiyo ikawa inatokana na kushindwa kujiimarisha kwenye ngazi ya chini ambako ndiko waliko watu wengi wanaoweza kujiunga katika vyama hivyo au kuviunga mkono.

Mtindo wa kuendelea kuvizia na kujitokeza katika uchaguzi bila kujiandaa, hauwezi kuvisaidia vyama vya upinzani, badala yake viongozi wangebuni mbinu za kufanikisha kushiriki katika uchaguzi na kupata matokeo chanya.

Yale ambayo yalikikumba Chama cha TLP, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, yangefaa kuwa fundisho kwa vyama vingine vya upinzani kwa kufanya maandalizi mapema kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, chama hicho kilikosa mgombea urais na badala yake kiliunga mkono mgombea wa CCM, kikidai kwamba hakikuwa na mgombea mwenye uwezo wa kupambana na wa CCM.

Hatua ya chama hicho kukosa mgombea urais, ni wazi kwamba hakikuwa na maandalizi tangu kumalizika kwa uchaguzi wa mwaka 2015 na kujikuta kikipeperusha bendera ya CCM kwenye nafasi ya urais.

Lengo la chama cha siasa ni kushika dola kwa njia halali ambayo ni kupitia sanduku la kura, hivyo ili chama kifanikiwe katika hilo, ni muhimu kuzingatia kuwa mwisho wa uchaguzi, ni mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi mwingine.

## Mtoto mwenye ulemavu aliyefungiwa ndani na wazazi apata ufadhili kusoma

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MTOTO Kulwa Thomas (14) mwenye ulemavu wa viungo, mkazi wa viwanja vya Mwadui, Manispaa ya Shinyanga, anayedaiwa kufungiwa ndani muda wote na wazazi wake amefunguliwa na kupewa msaada wa kusomeshwa shule.

Wazazi hao walikuwa wanamfungia ndani na kuamuacha bila nguo wanapokwenda katika shughuli zao mbalimbali.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya wenye ulemavu binafsi ya Brother's, iliyopo Kitangili Manispaa ya Shinyanga, Fransisco Bega, alifichua siri ya mtoto huyo kufungiwa ndani alipozungumza na vyombo vya habari alipofika nyumbani kwao kumuona.

Mwalimu huyo alizungumza na wazazi hao na kuwaomba wasimfungie badala yake wampeleke shule na yeye yupo tayari kumsomesha bure. Alisema alifika katika familia hiyo baada ya kupewa taarifa na wasamaria wema kwamba kuna mtoto mwenye ulemavu anayefungiwa ndani na wazazi wake.

"Nimesikitishwa sana na kitendo cha wazazi wa mtoto huyu kumfungia ndani, na nimemkuta akiwa mtupu kabisa huu ni ukatili na kuzaa mtoto mlemavu siyo mkosi ni bahati," alisema Bega.

"Mimi nipo tayari kumsomesha huyu mtoto bure katika shule yetu ya walemavu sababu namuona anafundishika, ila ninachoomba kwenu nyie wazazi mtoe tu nauli ya kumleta shule na kurudi," aliongeza.

Kwa upande wake mama wa mtoto huyo, Anastazia Gelard, alikiri kumfungia ndani mtoto wake, kwa maelezo kuwa hana mtu wa kumuachia, sababu dada yake na wadogo zake wanakwenda shule.

Aidha, alisema kutokana na ugumu wa maisha anaomba wasamaria wema wampatie mtaji afungue biashara ndogo nyumbani kwake ili apate muda wa kumlea mtoto huyo na kutomfungia ndani tena.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Luteni Josephine Mwambashi, akikata utepe kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo cha mafunzo ya kilimo cha Mwendakulima kilichojengwa kwa ufadhili wa kampuni ya Barrick, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri awashukia wenyeviti uuzaji kinyemela wa ardhi kwenye vijiji

**Na Munir Shemweta,** KILOSA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewajia juu na kutoa onyo kwa wenyeviti wa vijiji wilayani Kilosa, Morogoro wanaojihusisha na kuuza ardhi ya vijiji bila kufuata taratibu.

Dk. Mabula alitoa onyo hilo juzi alipozungumza na wananchi wa kata ya Dumila wilayani hapa akiwa katika ziara ya kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za ardhi ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa wakati wa ziara yake mkoani Morogoro hivi karibuni.

Wakati wa ziara hiyo, Rais Samia alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Dumila kuhusu migogoro ya ardhi waliyodai kuwa imekuwa ikisababisha kushindwa kuendelea na shughuli za uzalishaji mali.

Dk. Mabula alisema migogoro mingi ya ardhi imekuwa ikisababishwa na wenyeviti wa vijiji hasa katika ugawaji ardhi na kusisitiza kuwa jukumu hilo kwa mujibu wa sheria ni mkutano wa kijiji na si mwenyekiti.

"Naomba muelewe kuwa mwenyekiti wa kijiji haruhusiwi kugawa ardhi na yeyote atakayepewa ardhi na mwenyekiti wa kijiji basi ajue imekula kwake," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri alimwagiza Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro, Frank Minzikuntwe, kuwapitisha katika sheria ya ardhi ya usimamizi vijiji wenyeviti wa vijiji ili kuielewa na kusimamia vizuri ardhi katika maeneo yao.

"Kasimamieni vizuri vijiji vyenu na mhakikishe ardhi katika maeneo yenu inapangwa, inapimwa na kumilikishwa maana upangaji ardhi katika maeneo yenu utapunguza migogoro ya ardhi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, alimhakikishia Naibu Waziri Mabula kuwa atahakikisha sheria za usimamizi wa ardhi katika mkoa zinasimamiwa vizuri ili kuhakikisha migogoro ya ardhi inapungua au inakoma kabisa.

Dk. Mabula alianza utekelezaji maagizo ya Rais Samia kwa kufanya kikao cha ndani na viongozi wa wilaya ya Kilosa kwenye ofisi ya Kata ya Dumila na kuhusisha wenyeviti wa vijiji, watendaji wa mitaa, madiwani na wananchi waliowasilisha malalamiko kwa Rais.

Katika kikao hicho, wenyeviti wa mitaa wakiongozwa na madiwani walimweleza Naibu Waziri kuwa migogoro ya ardhi katika maeneo yao inahusisha mipaka kati ya vijiji, kubomolewa kwa baadhi ya nyumba za wananchi, kutopimwa baadhi ya vijiji, wananchi kuzuiwa kuendelea na shughuli za kiuchumi na wanaodaiwa wamiliki halali pamoja na mgogoro ya uvamizi wa maeneo.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Mabula aliagiza kuchukuliwa hatua kwa watumishi watatu wa wizara walioshindwa kuripoti katika kituo chao kipya cha kazi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

"Kama mtakumbuka tulifanya maamuzi (uamuzi) magumu (mgumu) kwenye mkoa wa Morogoro kwa kuhamisha asilimia 90 ya watumishi wa sekta ya ardhi na wapo watumishi watatu waliopangiwa kufanya kazi hapa Kilosa, lakini mpaka sasa hawajaripoti. Namwagiza Kamishna wa Ardhi awasiliane na Katibu Mkuu ili hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao," alisema.


halopesa
*150*88#

Ada za wateja

| Kiwango (TSH) | | Ada kwa mteja (TSH) | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kwenda HaloPesa | | | Kwenda Mitandao Mingine | | | Tuma kwa Namba Isiyosajiliwa | | | Kutoa Pesa | | |
| Kutoka | Mpaka | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Serikali | Makato ya Jumla | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Serikali | Makato ya Jumla | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Serikali | Makato ya Jumla | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Serikali | Makato ya Jumla |
| 100 | 999 | 10 | - | 10 | 10 | - | 10 | - | - | - | - | - | N/A |
| 1,000 | 1,999 | 20 | 10 | 30 | 35 | 10 | 45 | 350 | 10 | 360 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 20 | 16 | 36 | 35 | 16 | 51 | 380 | 16 | 396 | 300 | 16 | 316 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 27 | 77 | 70 | 27 | 97 | 475 | 27 | 502 | 400 | 27 | 427 |
| 4,000 | 4,999 | 55 | 56 | 111 | 85 | 56 | 141 | 530 | 56 | 586 | 500 | 56 | 556 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 100 | 230 | 180 | 100 | 280 | 710 | 100 | 810 | 780 | 100 | 880 |
| 7,000 | 9,999 | 130 | 125 | 255 | 180 | 125 | 305 | 790 | 125 | 915 | 780 | 125 | 905 |
| 10,000 | 14,999 | 320 | 320 | 640 | 500 | 320 | 320 | 1,250 | 320 | 1,570 | 1,200 | 320 | 1,520 |
| 15,000 | 19,999 | 320 | 610 | 930 | 500 | 610 | 1,110 | 1,250 | 610 | 1,860 | 1,200 | 610 | 1,810 |
| 20,000 | 29,999 | 360 | 960 | 1,320 | 550 | 960 | 1,510 | 1,5550 | 960 | 2,510 | 1,500 | 960 | 2,460 |
| 30,000 | 39,999 | 370 | 1,100 | 1,470 | 620 | 1,100 | 1,720 | 1,620 | 1,100 | 2,720 | 1,600 | 1,100 | 2,700 |
| 40,000 | 49,999 | 380 | 1,500 | 1,880 | 720 | 1,500 | 2,220 | 1,800 | 1,500 | 3,300 | 2,100 | 1,500 | 3,600 |
| 50,000 | 99,999 | 580 | 2,050 | 2,630 | 1,000 | 2,050 | 3,050 | 2,350 | 2,050 | 4,400 | 2,500 | 2,050 | 4,550 |
| 100,000 | 199,999 | 700 | 2,530 | 3,230 | 1,500 | 2,530 | 4,030 | 2,750 | 2,530 | 5,280 | 3,300 | 2,530 | 5,830 |
| 200,000 | 299,999 | 750 | 2,940 | 3,690 | 1,800 | 2,940 | 4,740 | 4,200 | 2,940 | 7,140 | 4,500 | 2,940 | 7,440 |
| 300,000 | 399,999 | 950 | 3,500 | 4,450 | 2,000 | 3,500 | 5,500 | 5,600 | 3,500 | 9,100 | 5,500 | 3,500 | 9,000 |
| 400,000 | 499,999 | 1,200 | 4,100 | 5,300 | 2,200 | 4,100 | 6,300 | 6,600 | 4,100 | 10,700 | 6,000 | 4,100 | 10,100 |
| 500,000 | 599,999 | 1,300 | 5,200 | 6,500 | 2,800 | 5,200 | 8,000 | 7,500 | 5,200 | 12,700 | 6,400 | 5,200 | 11,600 |
| 600,000 | 699,999 | 1,400 | 6,400 | 7,800 | 3,200 | 6,400 | 9,600 | 7,600 | 6,400 | 14,000 | 7,000 | 6,400 | 13,400 |
| 700,000 | 799,999 | 1,400 | 7,100 | 8,500 | 3,200 | 7,100 | 10,300 | 7,650 | 7,100 | 14,750 | 7,000 | 7,100 | 14,100 |
| 800,000 | 899,999 | 1,750 | 7,520 | 9,270 | 3,500 | 7,520 | 11,020 | 8,100 | 7,520 | 15,620 | 7,500 | 7,520 | 15,020 |
| 900,000 | 1,000,000 | 1,750 | 8,900 | 10,650 | 3,500 | 8,900 | 12,400 | 8,300 | 8,900 | 17,200 | 7,500 | 8,900 | 16,400 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 3,000 | 9,400 | 12,400 | 4,000 | 9,400 | 13,400 | 8,300 | 9,400 | 17,700 | 7,500 | 9,400 | 16,900 |
| Zaidi ya 3,000,000 | | 3,000 | 10,000 | 13,000 | 5,000 | 10,000 | 15,000 | 8,300 | 10,000 | 18,300 | 7,500 | 10,000 | 17,500 |

Halotel Tanzania Halotel_tanzania Haloteltz

216357801

HABARI KITAIFA

# Kampuni yachangia saruji, madirisha ujenzi zahanati

**Na Neema Sawaka,** MSALALA

ZAHANATI ya Kijiji cha Nyamigege, Kata ya Busangi wilayani Kahama imepatiwa msaada wa mifuko 40 ya saruji na madirisha 25 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi.

Msaada huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Kampuni ya Mabao Investment and General Pest Control Ltd (AMJ) kupitia Mkurugenzi wake, Abel Thomas.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Thomas alisema vifaa vyote vina gharama ya Sh. milioni 2.4.

Alisema kampuni yake imeamua kutoa msaada huo ili kuunga mkono juhudi za wananchi wa kijiji hicho waliojenga zahanati hiyo tangu mwaka 2011.

Diwani wa Kata hiyo, Alexander Mihayo, alisema msaada huo utasaidia kukamilisha ujenzi huo na kwamba zahanati hiyo itakuwa msaada kwa wananchi hao.

Mtendaji wa kata hiyo, Evamary Elias, alisema wananchi wa kijiji hicho wanatembea umbali wa kilomita zaidi ya tano kutafuta huduma za afya katika vijiji jirani.

"Wakazi wa kijiji hiki kila mwaka walikuwa wakitoa kipaumbele kwa zahanati hii ili kuhakikisha inakamilika na halmashauri tayari imetenga bajeti kwa mwaka wa 2021/2022 kiasi cha Sh. milioni 50 ili kukamilisha vitu vyote vinavyohitajika na kuanza kufanya kazi ya kutoa huduma kwa wananchi," alisema Elias.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Anthony Guta, alisema wananchi wanateseka kutafuta huduma za afya kwa kuwa hawana zahanati.

# Ardhi yaanza kutekeleza maagizo ya Rais Samia

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameanza kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero za ardhi katika Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro.

Akiwa njiani akitokea mkoani Morogoro katika ziara yake hivi karibuni, Rais Samia alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Dumila wilayani Kilosa, wakimweleza kuwa maeneo yao yana migogoro mingi ya ardhi jambo walilolieleza linalosababisha kushindwa kuendelea na shughuli za uzalishaji mali.

Dk. Mabula alianza utekelezaji maagizo hayo ya Rais kwa kufanya kikao cha ndani na viongozi wa Wilaya ya Kilosa wakiwamo wenyeviti wa vijiji, watendaji wa mitaa, madiwani pamoja na wananchi waliowasilisha malalamiko kwa Rais Samia.

Wakati wa kikao hicho, wenyeviti wa mitaa wakiongozwa na madiwani, walieleza migogoro ya ardhi katika maeneo yao kuwa ni ya mipaka kati ya vijiji, kubomolewa kwa baadhi ya nyumba za wananchi, kutopimwa baadhi ya vijiji, wananchi kuzuiwa kuendelea na shughuli za kiuchumi na wanaodaiwa wamiliki halali pamoja na mgogoro ya uvamizi wa maeneo.

Akizungumza na viongozi hao juzi, Mabula alieleza kuwa, migogoro mingi ya ardhi imesababishwa na wenyeviti wa vijiji hasa katika suala la ugawaji ardhi na kusisitiza kuwa mwenye mamlaka ya kugawa ardhi ya kijiji ni mkutano wa kijiji na siyo mwenyekiti wa kijiji na ardhi hiyo haitakiwi kuzidi ekari 50.

Alisema, suala la kupima mipaka ni la halmashauri kwa kutenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo na kuhakikisha vijiji vinapimwa na kupatiwa vyeti na alitaka utengaji fedha ufanyike kila mwaka.

Aidha, alisisitiza kwa kuwaeleza viongozi hao kuwa, suala la kuvamia mashamba na kukaa miaka 30 haijengi uhalali wa mwananchi kujiona mmiliki halali na kuongeza kuwa, kutokana na serikali kuwajali wananchi wake ndiyo maana inawafikiria waliovamia kwa kuwaachia sehemu ya mashamba.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro, Frank Mizikunte, aliwataka wananchi kuheshimu mhimili wa mahakama pale unapotoa maamuzi kuhusiana na migogoro ya ardhi na kusisitiza kuwa hakuna namna ya kukwepa maamuzi hayo.

Wilaya ya Kilosa imekuwa na migogoro ya ardhi kwa muda mrefu ikiwamo migogoro iliyohusisha wawekezaji wa mashamba makubwa walioshindwa kuendeleza kwa mujibu wa sheria jambo lililosababisha Rais Samia kufuta jumla ya mashamba 11 yenye ukubwa wa ekari 24,119 katika wilaya hiyo ili kugawiwa kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na uwekezaji.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan aliridhia pia ufufuaji wa mashamba 49 yenye ukubwa wa ekari 45,788.5 yaliyotaifishwa miaka ya nyuma huku na wananchi wakiwa hawana uhakika nayo ambapo Rais ameelekeza sehemu kubwa ya mashamba hayo kutumiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Sullivan Provost, Rachel Mwalukasa (wa tatu kulia), akikabidhi baadhi ya misaada kwa msimamizi wa kituo cha kulelea watoto wenye mahitaji maalum cha Child in the Sun, Padri Paul Raj, kinachoendeshwa chini ya Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi rasmi wa mpango maalumu wa shule hiyo wenye lengo la kuwafundisha wanafunzi wake kuwa na utamaduni wa kujitolea kusaidia jamii yenye mahitaji. **PCHA: JUMANNE JUMA**

# Wanafunzi waeleza siri kuingia 10 bora kitaifa

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Sekondari ya Baobab walioingia 10 bora kitaifa wamewapa siri wanafunzi wenzao jinsi ya kupata matokeo mazuri kama wao.

Wakizungumza na gazeti hili jana kwa nyakati tofauti, wanafunzi hao, Godwinner Joseph na Vailet Kahyoza, kila mmoja alielezea namna alivyoishi shuleni hapo hadi kufanya mtihani wa kitaifa uliowaingiza kwenye kumi bora kitaifa.

Joseph ambaye aliyeingia kwenye kumi bora kitaifa kwa kushika nafasi ya sita na namba tano kwa upande wa wasichana, alisema siri ya mafanikio ni kuzingatia masomo wakati wote na kusikiliza maelekezo ya walimu.

Alisema utulivu darasani ndiyo siri kubwa ya mafanikio ya mwanafunzi yeyote kwa kuwa amekuwa akifuatilia masomo kwa umakini na kuuliza maswali kwa walimu wake anapoona hajaelewa.

"Mimi napenda utulivu sana hasa wakati wa masomo kwa sababu najua elimu ndiyo ufunguo wa maisha na wazazi wangu wanatumia gharama kunisomesha nataka mwisho wa siku waone manufaa ya uwekezaji walioufanya kwangu hivyo nawashauri wenzangu wasome kwa bidii," alisema.

Kahyoza ambaye amekuwa watatu kwenye 10 bora kitaifa na kushika nafasi hiyo hiyo kwa upande wa kumi bora wasichana, alisema bidii ya masomo na mazingira bora ya kujisomea yamekuwa mchango mkubwa kwenye mafanikio yake ya kitaaluma.

Alisema wanafunzi wanapaswa kuzingatia masomo ili waweze kufanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa kwasababu wazazi wamekuwa wakijinyima na kugharamia masomo yao na kwamba wanasikitika wanapoona matokeo mabaya ya watoto wao kwenye matokeo ya kitaifa.

Naye Mkuu wa shule hiyo, Venance Hongoa, alisema wanafunzi wote 337 wa shule hiyo waliofanya mtihani wa kidato cha sita mwaka huu, wamefanikiwa kupata sifa za kujiunga na vyuo vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi na wameingiza wanafunzi wawili 10 bora kitaifa.

Alisema kwenye matokeo hayo wanafunzi 62 wa shule hiyo wamefaulu kwa daraja la kwanza, 163 daraja la pili, 108 daraja la tatu na wanne wamepata daraja la nne na hakuna aliyeanguka kwenye matokeo hayo.

Alitaja siri ya kufaulisha idadi kubwa ya wanafunzi kuwa ni bidii ya walimu ambao hujituma usiku na mchana kuhakikisha wanafunzi wote wanajiandaa vyema kwa ajili ya mitihani ya ndani na ile ya kitaifa.

"Siku zote sisi tunachukua wanafunzi wenye ufaulu wa kawaida sana na hao wengi tuliochukua ni wale waliofanya usaili na wakakosa nafasi shule zingine sisi tukawachukua na kuwatengeneza na sasa wamefaulu vizuri sana tunajivunia kwa hilo," alisema.

# Uzalishaji korosho kuongezeka kwa 42.8%

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Korosho imesema ina mpango wa kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 300,000 za sasa hadi 700,000 ifikapo mwaka 2025/26.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Francis Alfred, alisema hayo kwenye banda lao la Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu kama Sabasaba yaliyoanza Juni 28, mwaka huu na kumalizika jana.

"Wakati tukifikiria kwenda kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi, tunataka pia kuhamasisha uongezaji wa thamani katika zao hili la korosho, kwa hiyo lengo letu la kushiriki maonyesho hayo ni kuonyesha wadau na washiriki wa maonyesho hayo kwamba zipo fursa nyingi za uongezaji wa thamani katika zao hili," alisema Alfred.

"Cha kwanza ni katika kuongeza ubanguaji, sasa hivi tunabangua wastani wa asilimia 10 ya korosho zetu zote ambazo tunazizalisha, kwa hiyo tunataka kuongeza ubanguaji ufike asilimia 60 kufikia mwaka 2025/26, kwa hiyo hapa tunaonyesha wadau mbalimbali fursa zilizopo kwenye upande wa ubanguaji wa korosho , tuuze zaidi korosho iliyoanguliwa kuliko kuuza korosho ghafi  na tukifanya hivyo tutakuwa na uhakika zaidi wa soko la korosho," alisema Alfred.

Alisema kufanya hivyo kutaongeza uhakika zaidi wa soko la korosho kwa sababu wataweza kuuza katika nchi nyingi kuliko ilivyo sasa hivi ambapo wanategemea soko kutoka katika nchi mbili ambazo ni India na Vietnam.

Pia, alisema wanataka kupanua wigo wa soko kwa kubangua korosho na kuziuza katika nchi za Marekani, Bara la Ulaya, Mashariki ya Kati, China, Uarabuni, Bara la Afrika.

"Lakini tunataka kupanua soko la ndani, sasa kwa walaji wa soko korosho la hapa nchini ambalo bado ni dogo sana kwa sababu ya bei, lakini tukiongeza ubanguaji bei zitashuka na ulaji wa korosho nchini utaongezeka," alisema Alfred.

Alisema Julai 7, mwaka huu watakuwa na siku maalum ya kugawiwa korosho bure washiriki wa maonyesho hayo, na kwamba lengo likiwa ni kuhamasisha watu wale korosho ili wapate manufaa ya zao hilo.

"Tunataka zao la korosho liwe na manufaa zaidi katika jamii kwa maana kwamba na njia pekee ni wadau mbalimbali kushiriki katika mnyororo thamani wa zao hili kuanzia shambani na uongezaji wa thamani wa bidhaa mbalimbali zinazotokana na zao hilo.

Domina, Mkangara, Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Udhibiti Ubora wa Bodi ya Korosho, alisema wameshiriki katika maonyesho hayo kuonyesha Watanzania fursa mbalimbali zilizopo katika zao hilo.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiriba, Kata ya Kiriba, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiwa kwenye masomo ya sayansi kwa vitendo, katika maabara ya shule hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanawake waitwa mafunzo ujasiriamali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Kibaha Mjini mkoani Pwani, Elina Mgonja, amewataka wanawake kuendelea kuhudhuria kwenye mafunzo ya wajasiriamali ili waweze kujiajiri.

Akizungumza na Nipashe, Elina alisema mafunzo yanayoendelea kwenye Ofisi ya CCM Kibaha Mjini yanaambatana na kutangaza bidhaa za wajasiriamali zinazotengenezwa.

Aliwataka wanawake wenye nia ya kujikomboa kiuchumi kufika kupata mafunzo hayo ili waweze kutengeneza bidhaa na kuziuza kwenye masoko mbalimbali.

"Hili darasa la wajasiriamali ni endelevu, tumejipanga kumkwamua mwanamke asikae nyumbani apate alimu atengeneze bidhaa zake na kuziuza sehemu yoyote kwa kufanya hivi tutajikwamua kiuchumi," alisema.

Elina alisema pia kuna ujenzi wa duka la bidhaa za wajasiriamali ambalo linajengwa katika ofisi hiyo.

## H/shauri yakusanya mapato kwa mfumo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga imefunga mfumo wa ukusanyaji wa mapato (LGRCIS) wenye thamani ya Sh. milioni 112. 7, kwa lengo la kujua halmashauri hiyo inakusanya kiasi gani kwa siku, mwezi hadi mwaka.

Kadhalika, halmashauri hiyo inatarajia kuweka mifumo ya simu za ndani, vifaa vya mikutano, kamera, vifaa vya mahudhurio ya watumishi na ifikapo Julai 30 mwaka huu wanatarajia kutumia Sh. milioni 10.7 kati ya Sh. milioni 112.7 zilizotengwa.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Juma Benjamin, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa za ujenzi wa mfumo huo kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Luteni Josephine Mwambashi.

Alisema mfumo huo utasaidia kudhibiti mapato yanayokusanywa ikiwa ni pamoja na kuwezesha matumizi shirikishi ya rasilimali za TEHAMA.

Aliongeza kuwa mfumo huo utaongeza usalama wa taarifa mbalimbali za serikali kwani mtandao huo utalinda taarifa zote zinazoingia ndani ya taasisi.

# TALIRI kujikita teknolojia mpya sekta ufugaji

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), imesema itaendelea kubuni teknolojia mpya za kuboresha na kuinua sekta ya ufugaji ili kuhakikisha inaleta tija zaidi kwa wafugaji na kwa uchumi wa nchi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TALIRI, Prof. Erick Komba, katika banda lao kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF).

Alisema zipo teknolojia nyingi ambazo wamezibuni zinazolenga kuboresha zaidi sekta ya ufugaji ikiwamo kuwa na ng`ombe wa kisasa aina ya Mpwapwa ambaye anazalisha maziwa mengi na nyama nyingi tofauti na ilivyo kwa ng`ombe wa asili.

"Baada ya kubuni na kubaini tija zinazotokana na huyu ng`ombe aina ya Mpwapwa, tunachofanya ni kusambaza kwa wafugaji ili nao wakimfuga wapate tija kubwa kwa kupitia maziwa na nyama na kuboresha maisha yao," alisema Prof. Komba.

"Kwa hiyo kila mwaka tunasambaza kama madume 150 kwenye mikoa na halmashauri mbalimbali za kifugaji ili watu wayatumie kuzalishia ng`ombe wa kienyeji ili anayezaliwa awe amechukua baadhi ya sifa zinazofanana na huyu anayetoa maziwa na nyama nyingi, kwa hiyo unakuwa unamwongezea yule wa kiasili uwezo wa uzalishaji."

Aliwashauri wafugaji kuacha ufugaji wa mazoea na badala yake kufuga mifugo ambayo itawaletea tija.

"Ushauri wangu mkubwa kwa wafugaji ni kwamba waache ule ufugaji wa mazoea, ufugaji ambao unakuwa na mifugo mingi lakini inakuwa haina tija, kwa mfano mtu anakuwa na ng`ombe wa kienyeji 20. Lakini unakuta kila mmoja anatoa lita moja ya maziwa, wakati ukiwa na ng`ombe mmoja huyu wa kisasa aina ya Mpwapwa anakupa lita nane(8) ambazo ni kama zinazotoka kwa ng`ombe nane wa kienyeji."

"Kwa hiyo inabidi tuhame kutoka huko kwa sababu itatusaidia kufuga ng`ombe wenye tija na itapunguza migogoro ambayo imekuwa ikitokea ya wakulima na wafugaji."

Pia, Prof. Komba aliwataka wafugaji kuingia kwenye teknolojia ya kisasa ya kupanda majani ya malisho bora kwa mifugo yao.

"Kwa hiyo hata vijana au wamama nao wanaweza kuiona hii fursa wakawekeza kwenye teknolojia hii na watafanya biashara sana."

# Bajeti kushusha bei vileo kunavyoinyonga nguvu kazi



Ukurasa 13



Ukurasa 14

## Wataua kisa? Eti kumlinda Zuma

siasa

JUMATANO JULAI 14, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# ANAYEKATAA KATIBA YUKO MBALI NA WANANCHI – WARIOBA

Na Mwandishi Wetu

JAJI Joseph Warioba, amesisitiza kuwa Tanzania imefika hatua kubwa ya kuwa na katiba mpya na kwamba anayesema katiba si kipaumbele atakuwa mbali na wananchi.

Katika kipindi cha Dakika 45 kilichorushwa na ITV Jumatatu wiki hii Mwenyekiti wa Tume ya Kukusanya Maoni ya Wananchi anasema: "Mtu asije akasema katiba siyo muhimu wakati wananchi wanasema ni muhimu. Tusije kudharau wananchi. Anayesema katiba siyo muhimu atakuwa mbali na wananchi."

Anakumbusha kuwa ni kwa sababu taifa limefikia hatua muhimu kupata katiba hiyo na kinachotakiwa ni kutafakari nini kinafanyika na kwa vipi na lini ili kukamilisha suala hilo.

"Tumewauliza wananchi wakasema Katiba ni muhimu zaidi, hivyo mtu asije akasema Katiba siyo muhimu."

Anasema sheria ilitungwa ikaunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Sheria ikaelekeza kupata maoni ya wananchi, tume ikazunguka nchi nzima kuyakusanya.


Anasema maoni hayo ndiyo yaliyomo kwenye rasimu ya Tume na ndiyo yaliyochukuliwa na Bunge Maalumu la Katiba ambayo yalitokana na maoni ya wananchi.

Anakumbusha kuwa ni mara ya kwanza serikali ilipata maoni ya wananchi kwani katiba za zamani hazikuwa zikuwauliza raia maoni yao.

"Ni wakati mmoja mwaka 1983 CCM ilipopatiwa mapendekezo ya urekebishwa katiba ikipewa miezi tisa ili wananchi wazungumze. Walitoa maoni yao ambayo ni muhimu lakini hayakuwa na haki za binadamu."

Anafafanua kuwa wakati ule hakukuwa na masuala ya haki za binadamu kwenye katiba na wananchi wakasema ni muhimu sana yawekewe kwenye katiba.

Anasema haki za binadamu ziliingizwa na wananchi kwenye katiba na safari hii waliyazungumza zaidi.



Jaji Warioba mtetezi wa maoni ya wananchi kwenye Katiba mpya. **PICHA: MTANDAO**

### RAIS HAJAIKATAA

Anasema alimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye katiba hajakataa Katiba anachozungumzia ni muda, hajasema lini kazi hiyo itafanyika.

"Naona tufikirie sasa ni lini tutaikamilisha na tutumie utaratibu gani, mwaka 2014 ilikuwa baada ya Bunge Maalumu twende kupata maoni ya wananchi, lakini mazingira hayakuwa mazuri."

Jaji Warioba anasema sasa muda umekwisha inabidi katiba hiyo ifanyiwe marekebisho. Bunge maalumu limekwisha na kuna ulazima wa kurekebisha mfano, katiba ilitamka kuwa ni ya mwaka 2014, muda ambao ingekuwa ianze wakati ule lakini haikuthibitishwa na wananchi ni lazima mwaka ubadilike.

Anasema hilo linawezekana kwa sababu kuna sheria ya mabadiliko ya katiba, ilitungwa na kufanyiwa marekebisho karibu mara tatu ndani ya mwaka 1.5. hivyo inaweza kurekebishwa tena.

### KATIBA NI IPI HASA

Katika mazungumzo yake anahoji wapo wanaotaka Katiba ya Wananchi na kuuliza

wanataka katiba ipi hasa ile ya wananchi au ya wabunge?

"Wanachozungumza ni Tume Huru ya Uchaguzi, rais kuchaguliwa na zaidi ya asilimia 50 ya wapigakura, matokeo ya urais kupingwa mahakamani na kuwa na mgombea huru. Haya ni mambo muhimu lakini ndiyo ulikuwa msisitizo wa wananchi au kulikuwa na mengine? Anahoji.

Anasema wananchi walikuwa na mambo mengine mfano kuwapo mmomonyoko mkubwa wa maadili kunakosababisha rushwa kubwa, ufisadi, kukosekana uwajibikaji.

Anasema walitaka jambo hilo liingie kwenye katiba na Tume ikakubali hivyo ni lazima uanze utaratibu wa kujenga tunu za Mtanzania ili ijulikane Mtanzania ni mtu gani? Awe anayejali utu, hana ubaguzi, mzalendo na mwadilifu, anayependa umoja, uadilifu, amani lugha yake ya taifa lake.

INAENDELEA UK. 14

# Chongolo aanza na kutoa mwelekeo CCM anayoitaka



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Beatrice Shayo**

TUMEKUBALIANA katika mikakati yetu kuwa ifikapo mwakani tutashusha waraka ngazi ya chini. Kwa atakayetaka kuchukua fomu za uongozi masharti yake tutataka awe na muktasari wa vikao alivyovifanya kwenye mashina."

Ni maagizo ya Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, anapozuru Zanzibar katika ziara ya kujitambulisha kwa wana-CCM na viongozi hivi karibuni .

Anaongeza kuwa vikao vya mashina ni muhimu kwa wananchi kwani vinatatua kero zao na kuwaelimishana masuala mbalimbali yanayohusu maisha na maendeleo yao.

Chongolo anasema kukosekana kwa vikao hivyo ni hatari na watajikuta wanazalisha viongozi ambao hawana sifa huku kero za wananchi zikikosa utatuzi.

"Tunatakiwa kukutana kuonyana na kunyoosheana vidole kwa watoto wetu ambao wanapotoka kimienendo na maadili. Hapo ndipo tunajuana mtoto kwa mtoto, baba kwa baba," anasema Chongolo.

Anasema kumekuwapo na mambo mabaya yanayofanywa na watoto ama vijana kama udokozi, wizi na kutoroka shule na kutaka vikao hivyo vitumike kuwarekebisha ili wafuate njia sahihi.

> "Tuache kutengeneza safu za uongozi chama hiki ni kikubwa kuliko kutengenezeana mazingira. Tuna chama ambacho kina historia ndefu tumejijenga katika misingi imara tuache kujitengenezea mazingira hatarishi kwa kuandaa safu ambazo hazidumishi uimara wa chama," anasema Chongolo.

"Tusipokaa vikao ni hatari kwetu sisi wenyewe tutabakia kwenye mitandao kulalamika siyo nzuri, mambo hayaendi lakini nani wa kwanza kuwa mlinzi wa nchi yake ni sisi wenyewe. Kila mmoja kwa eneo lake ukisimama nchi yetu itakuwa salama," anasema KM.

Anawaasa kuwa wasipofanya hivyo watawapata viongozi 'duni' na baadaye kulaumiana. "Tutapata viongozi ambao tutakuja kuambiana ... wewe uliyetoka huku tunataka utuonyeshe ushahidi namna ambavyo unashiriki na ushahidi ni vikao."

Anasema watu ambao wanaonekana ni viongozi bora wahamasishwe kuchukua fomu na kugombea nafasi za uongozi kwa kuwa CCM ina watu wengi ambao wanafaa kuongoza.

Anasema mara nyingi viongozi ambao wanafaa hawajiweki mbele katika kutafuta madaraka ni vyema wakashawishiwa kugombea nafasi.

Chongolo anaeleza kuwa kiongozi ni yule ambaye ukimwangalia unaona tabia yake, mwenendo wake, kusema kwake, mwonekano wake, heshima na matendo yake, namna anavyoshirikiana na wenzake, anavyojihusisha katika maendeleo, alivyo na uchungu wa mambo ya wenzake huyu anafaa kuongoza.

"Wahamasisheni watu wa aina hiyo achaneni na wale wengine eti wa uwezo kwa kusaidia kupata kilo ya samaki ama ya nyama. Sifa ya uongozi haitengenezwi kwa kuwa na uwezo wa kutoa kilo ya unga," anaonya Chongolo.

**KUJIPANGIA VIONGOZI**

Changolo anasema kumekuwa na mtindo wa watu kutengeneza safu za uongozi kufanya hivyo ni kupatikana viongozi wasio na sifa.

Anasema kazi yao ni kuhakikisha wanaendeleza na kukiacha chama kikiwa salama kwa kuzingatia yale ambayo yalifanywa na waasisi.

"Tuache kutengeneza safu za uongozi chama hiki ni kikubwa kuliko kutengenezeana mazingira. Tuna chama ambacho kina historia ndefu tumejijenga katika misingi imara tuache kujitengenezea mazingira hatarishi kwa kuandaa safu ambazo hazidumishi uimara wa chama," anasema Chongolo.

**CHAMA KIPO IMARA**

Chongolo anasema CCM ipo imara na haitayumba na mikakati yao ni kutekeleza ilani na kuongeza: "Tupo imara kuhakikisha tunasukumu gurudumu la chama tupo imara hatutayumba tunahakikisha kila kilichopo kwenye ilani yetu ya 2020/25 kinatekelezwa," anasema.

Chongolo anawaambia wana CCM kuwa hata yale ambayo ni ahadi binafsi za wagombea wao Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Dk. Hussen Mwinyi wa Zanzibar pamoja na viongozi wote waliozunguka nchi nzima kunadi na kuomba kura ili kuaminiwa mwaka 2020 zinakwenda kutekelezwa ili kuondoa maswali mwaka 2025.

Anasema utekelezaji wa ilani na mikakati yao waliyojipanga ifikapo mwaka 2025 watarudi na ushindi wa kishindo zaidi ya mwaka jana.

**KUMUUNGA MKONO RAIS**

Chongolo anasema kuna wajibu wa kuunga mkono viongozi wa nchi akimtaja Mwenyekiti wa CCM na Rais Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Rais Dk. Hussein Mwinyi.

"Tuna wajibu wa kuwasemea, kuwatetea, kuwalinda hiyo ni kazi yetu kwa sababu bila kuwalinda wakitokea watu wakaleta chokochoko ilani yetu haitaenda kwa kasi tunayoitegemea," anakumbusha.

Anataka vijana wakae imara katika nafasi zao na watumie muda wao kuwatetea, kuwalinda na kuwasemea viongozi hao wanafanyakazi kubwa kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

**KUONGEZEKA UNYANYASAJI**

Chongolo anasema vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia vimekithiri na hakuna budi kuwafichua wote wanaoendeleza vitendo vya namna hiyo.

"Tumepewa chombo ambacho kinasimamia haki na kulinda maslahi ya raia na moja kuzuia na kupinga udhalilishaji, kazi yetu ni kuwafichua kwafikisha mbele ya sheria tusiwalee wala kuwachekea madhara yake sio madogo."

Anasema athari zake ni zinasababisha watu kutokuwa na amani na maisha yao yanaumizwa hasa ya watoto."Natoa wito kwa kila mmoja katika sehemu yake kuhakikisha anasimama na kupinga vita unyanyasaji huu wa kijinsia,"

**KUJIKINGA NA CORONA**

Chongoro anawaomba wananchi kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona na kujikinga na maradhi hayo ambayo hapa Tanzania yapo na pia nchi zilizopakana na Tanzania hazipo shwari.

"Hutuwezi kujiachia, maradhi yapo nchini, majirani zetu hawapo salama na sisi pia tusikae kienyeji tujilinde na madhara ya ugonjwa huu. Magonjwa ya namna hii ikiwamo corona yanaathiri nguvu kazi na kutupunguza idadi ya watu inapofika kwa wananchi wetu."

Anasema ni muhimu kujiepusha na mazingira ambayo yanayowaweka watu katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo.



Ulevi unaweza kuongeza mapato lakini, athari yake inaweza kuumiza nguvu kazi hasa vijana ambao watawekeza kwenye kuabudu pombe. **PICHA: MTANDAO**

NYAKATI ZA ULEVI

# Bajeti kushusha bei vileo kunavyoinyonga nguvu kazi

**Na Dk. Felician Kilahama**

KUNA msemo 'subira yavuta heri' hata hivyo kwa wenye uovu hakuna cha kuvuta heri. Kadri siku zinavyosonga mbele wengi wanavutika na masuala ya kuwa na fedha, mali na utajiri.

Wapo wanaozama kwenye starehe zikiwamo ulevi wa kupindukia, ni sehemu ya mambo yanayowagusa wengi.

Wanakosa upendo kwa Mungu na kwa taifa wakijikita zaidi kwenye ubadhirifu, wizi, udanganyifu fedha, starehe, ulevi na mambo yanafanana na hayo.

Hali ilivyo sasa inaashiria kuwa nyakati hizi ni za uovu na kuna dalili nyingi za kuthibitisha hayo kwa mfano kitendo cha kuchochea ulevi kwa kushusha bei ya pombe ni mojawapo ili ulevi ujitukuze kupitia kunywa zaidi.

Kadhalika, ubinafsi unazidi kwa wengi kuonekana kuwa wako tayari kukiuka maadili kwa faida binafsi bila kujali maslahi ya taifa au kumkosea Mungu.

Kutukana, kukejeli, kutumia mitandao ya kijamii vibaya, udanganyifu kugeuza uongo kuwa ukweli mathalani kushinikiza na kuendekeza ngono za jinsia moja ni baadhi ya matukio.

Mfano zipo ndoa za jinsi moja kama ushoga kwa madai kuwa ni kupendana kwa dhati, wizi na ubadhirifu wa mali za umma, kutokujaliana, ndoa na familia nyingi kukosa amani ya kweli. Hayo na mengineyo mengi siyo dalili njema kwa ustawi wa taifa pia ni dalili za uovu kutaka kuisambaratisha jamii.

Ni wakati wa kujiuliza walikosea wapi na taifa linaelekea wapi kimaadili? Kwa kujikita katika kupata fedha na kupitia fursa za ulevi na anasa uovu unazidi.

**BAJETI NA POMBE**

Baada ya bunge kupitisha bajeti ya serikali, awamu ya sita hivyo kuanza mwaka wa fedha wa Julai 1, 2021 ni jambo jema na ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi ya kijamii na kiuchumi.

Kwa Wizara ya Fedha ambayo ndiyo mamlaka inayowajibika katika kusimamia mapato na matumizi halisi ya bajeti ya serikali inawajibika ipasavyo kufuatilia na kusimamia matumizi sahihi ya fedha za umma.

> “Lakini pamoja na kuyasema hayo dukuduku moyoni mwangu na wengine linahusu mamlaka au serikali kushusha bei za vinywaji hasa vileo ambavyo kitaalamu huitwa 'intoxicating drinks'.

Ingawa wizara zote pamoja na serikali za mitaa zinawajibika kusimamia matumizi bora ya fedha za umma, lakini Wizara ya Fedha inabaki kuwa mhusika mkuu.

Watanzania wote waendelee kuliombea taifa na viongozi ili hekima za kimbingu zitumike kufanya maamuzi yaliyo sahihi kwa faida ya wengi.

Lakini pamoja na kuyasema hayo dukuduku moyoni mwangu na wengine linahusu mamlaka au serikali kushusha bei za vinywaji hasa vileo ambavyo kitaalamu huitwa 'intoxicating drinks'.

Wengi hawapati picha sahihi nini kimejiri mpaka kuamua kupunguza bei mfano pombe zinazozalishwa nchini ikiwamo bia?

Inawezekana hatua hiyo inafanyika kuvutia wanywani au walevi wengi ili mamlaka iweze kukusanya fedha zaidi kuliko kuweka tozo kubwa na wanywaji wakawa wachache.

Ni kweli taifa linahitaji fedha za kutosha kuweza kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kuinua uchumi na hali za maisha. Hata hivyo, nimekuwa kitembelea maeneo mengi nchini mijini na vijijini; lakini sijawahi kushuhudia sehemu za kuuza vileo hususani baa na stoo za pombe zikiwa zimefungwa kwa kukosa wanywaji.

Utitiri wa baa na stoo zilizopo kwenye maeneo mengi nchini ni hatari, hali inatisha kwa wanywaji kuanza tangu asubuhi bila kujali saa za kazi.

Licha ya kwamba kuna sheria na taratibu kuwa pombe zianze kunywewa saa 10 hasa mijini na majini ikiwamo Dar es Salaam, bado ulevi unaanza alfajiri na mapema.

Cha kusikitisha vibanda vingi na kioski vimejaa pombe na huuzwa wakati wote na huenda wahusika hawalipi kodi ambayo serikali inailenga baada ya kushusha bei ya kilevi hicho.

**NGUVU KAZI HOI**

Bei ya vileo imeshuka maana yake ni nini? Inamaanisha kwamba taifa litakusanya fedha nyingi na wakati huohuo, watu wake hasa nguvu kazi vijana, liwe ni kundi la wanywaji hivyo kujenga taifa dhaifu lisilo na afya.

Iwapo unywaji ulikuwa unaendelea wakati bei ilikuwa haijashuka sasa imeshuka baa na stoo zifurike inamaanisha ulevi utapandisha mabega juu.

Kama ndiyo itakayokuwa hali halisi litakuwa jambo la kusikitisha maana serikali inawaza kupata fedha nyingi lakini matokeo yake uovu ulevi ukaongezeka.

Wakati huohuo bei za mafuta hasa petrol na dizeli zikipandishwa kwa kuongeza tozo kwa nia ya kutumia fedha zitakazokusanywa kujenga na kuimarisha barabara na miundombinu vijini.

Nia ni njema lakini gharama za usafiri pia zitapanda mwisho wake ni huyo mlengwa kuumia zaidi kwenye kila sekta kwani nishati inahusu shughuli zote za maendeleo.

Ingawa taifa limo katika kipindi kigumu cha kujiletea maendeleo na kuvumilia maumivu kwa kipindi fulani na barabara vijijini zikaimarika, elimu ikaboreshwa na huduma za afya na maji zikawa bora nchi itakuwa imepiga hatua inayotarajiwa.

**KULETA MADHARA**

Pamoja na hayo, kushusha bei za vileo kutachochea ulevi na madhara kwa jamii yatakuwa makubwa zaidi. Nyakati hizi watu wengi hasa vijana wamejitokeza kuwa watumiaji wa vileo kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Kwa mtazamo wangu ingelikuwa heri iwapo bei za vileo zingebakia kama zilivyokuwa. Ongezeka la tozo ya Shilingi 100 kwa kila lita moja ya mafuta kwa lengo la kuimarisha barabara vijijini likapata maelezo na wananchi wakaelimishwa ipasavyo kwamba maendeleo halisi yatatokana na nguvu zao za ndani badala ya kutegemea misaada na mikopo.

Hali hiyo ingeeleweka na kujifunga mikanda kwa minajili ya kujiletea maendeleo endelevu kwa faida ya wote.

Kimsingi tozo ya Shilingi 100 kwa lita moja isingekuwa chanzo kikuu cha kuumiza Watanzania. Isipokuwa tangu zogo la COVID-19 liikumbe dunia, uzalishaji wa bidhaa za mafuta umekuwa ukishuka na kusababisha bei zake katika soko la dunia kuongezeka mno.

Kimsingi, kupunguza bei za vileo kwa mantiki ya kupata mapato zaidi huku nchi ikichochea ulevi uongezeke suala hili halijakaa vizuri ingawa uovu na ulevi utawanasa wengi.

Ni vyema viongozi na taifa litumie hekima walione hilo na ikiwezekana hatua zichukuliwe kulirekebisha kwa faida ya wote.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Wataua kisa? Eti kumlinda Zuma



Zuma akiwa kizimbani siku za hivi karibuni. **PICHA MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma, anajitokeza mara ya pili kuwa gumzo la kitaifa nchini humo. Kwanza tatizo lilianzia wakati wa kampeni ya mtangulizi wake, Thabo Mbeki, akiwa Rais wa pili wa Afrika Kusini baada ya Mandela, alikitaka chama tawala kisiruhusu aingie ikulu.

Alitaka ANC ifanye kila kinachoweza kuzuia Zuma kuingia madarakani kwani alimfahamu fika na kile anachoweza kufanya endapo atakuwa kiongozi.

Hata hivyo, jamii haikuwa upande wake. Watu walimuona Mbeki kama msomi wa kabila tofauti mwenye majivuno, anayewabeza wasiofika vyuo vikuu kama Zuma, hivyo wakakataa ushauri wake. Mmoja wa wale waliobeba mabango na kutoa tahadhari kali kuionya ANC isiweke vizuizi kwa Naibu Rais Zuma kuchukua nafasi kubwa ya kuongoza taifa hilo ni Julius Malema.

Wakati huo Malema akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa ANC. Watu walimwona Zuma kama mwakilishi wa uzalendo wa kina, mshiriki mkuu wa ngoma za Wazulu, mtu wa watu, anayejua kile wasomi wanachokijua bila kuhudhuria vyuo vikuu wanavyopitia.

Swali kama ana wake wangapi? Liliulizwa. Baadhi walihoji, lakini jibu lake likawa ni kumsifia kuwa ni kawaida kuwa nao wengi.

Kimsingi kinachotokea leo ni sawa na kusema Afrika Kusini ilivuna na inaendelea kupata kile ilichopanda kwa upande mmoja kwani utawala wa Rais Zuma ulisheheni yale ambayo mtangulizi wake aliony a.

Kwa hiyo, ukaanza ukinzani mwingine ndani ya ANC ambao haukutilia maanani kuwa Zuma hakuwa mgeni kwao, hivyo ilibidi kuwe na mwelekeo wa kisiasa kwa suala hilo.

Tatizo ni kuwa sheria za Afrika Kusini ni sawa na Ulaya, rais akiondoka madarakani hana ulinzi wowote kwa kile alichokifanya, tofauti na nchi kadhaa za Afrika ikiwamo Tanzania zinazomlinda mstaafu ili asishtakiwe kwa kumpa kinga.

Pale ambapo rais akiondoka madarakani hana ulinzi, uthabiti wa kisiasa unakuwa na changamoto na ugomvi unaweza kuzuka.

Kwa upande mwingine suala siyo Zuma alifanya nini akiwa madarakani, au undani wa kilichomfikisha kotini, lakini dai la kuidharau mahakama kwa kutohudhuria kwenye kesi.

Aidha kutoonekana kwenye upelelezi kwa zaidi ya miaka ya kula rushwa katika kandarasi za simu kwa maofisa wa serikali ni mambo yanayomuweka matatani.

### KINGA KIKATIBA

Suala halisi ni kama Afrika Kusini ilivyo ina haja ya katiba inayofanana na Ulaya au nchi nyingine za Afrika.

Ukiangalia gharama inayotumika kuendesha kesi hiyo, na hasara ya kuchomwa maduka na magari na wafuasi wake, unapata picha kuwa Afrika Kusini katiba yake inahitaji kutazamwa.

Kinachooneka ni kama kusema hili ni koti la mbuzi, hivi mnyama huyu anavaa koti? Hapo ndipo watu watamshangaa wanapomuoa mbuzi amevaa koti ndicho kinachotokea Afrika Kusini hivi sasa. Kwa kujisahaulisha kuwa walisema kwa nguvu zote kuwa Zuma ni mtu wa watu.

Kwa Tanzania itakumbukwa kuwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliwahi kuzungumzia suala kama hilo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Agosti 10, 1978.

Alikuwa akijibu swali aliloulizwa kwanini aliondoa serikali huru ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akaweka ya Umoja wa Vijana wa CCM?

Uongozi huo ulikuwa ikisutwa katika taarifa za 'mzee panchi' zilizokuwa zinabandikwa juu sana kwenye kuta za majengo yakiwamo maeneo ya kulia chakula na mabweni.

Vijana wa CCM waliitwa 'hogs' au nguruwe, wasio na akili tena walafi.

Jibu la Mwalimu likawa kila nchi ina uongozi au serikali inayoistahili ('every country has a government it deserves).

Kwa maana hiyo Afrika Kusini imekuwa na kiongozi inayeistahili, endapo alikuwa hafai au hakufikia matazamio ya sehemu kubwa ya wananchi, ingebidi waridhike kuwa ameachia ngazi, nchi iende mbele.

Si visasi au kesi za kutaka kuthibitisha nadharia za Ulaya kuwa 'hakuna aliye juu ya sheria,'.

Hawapendi kiongozi mkuu na mlalahoi wote wakamatwe na koplo wa polisi, wakiamini kuwa huko ni kuidhihaki taadhima ya watu kwa kiongozi wao. Hata Baraza la Senate la Marekani lilikataa kupiga kura kumtia hatiani aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Donald Trump, kuchochea uasi na uvamizi wa Bunge (Capitol Hill) licha ya ushahidi kubainisha.

### KINGA NI MUHIMU

Tatizo la Zuma pia linachangia katika mjadala wa katiba mpya hapa nchini, na ni mwendelezo wa mijadala ya kitaaluma kuhusu chanzo cha katiba inayofaa kwa nchi za Afrika na hata sehemu kubwa ya nchi zinazoendelea. Ule msemo wa 'yaliyopita si ndwele tugange yaliyomo na yajayo' siyo utumike tu katika mahusiano binafsi ila hata uthabiti wa siasa nchini.

Kuwa kinga zikiondolewa kwa vile wako watu wanaopania kulipa visasi kwa yasiyoridhisha. Hata hivyo ni suala ambalo linabidi kutazamwa na kuangaliwa kwa jicho na macho makali zaidi ili kulinda uthabiti wa nchi na pia kulinda maadili na matumizi bora ya ofisi.

## ANAYEKATAA KATIBA YUKO MBALI NA WANANCHI – WARIOBA

**INATOKA UK. 11**

Aidha, anasema walizungumza kuhusu haki za binadamu na kutaka kuheshimu na kuzizingatia.

"Lakini wanaozungumzia katiba ya wananchi hawataji hayo wanataja yale yanayowaletea madaraka. Ni lazima tuyaangalie kabla hatujairudisha kwa wananchi kuiidhinisha." Anasema.

Anaongeza kuwa kuna mengine mengi kama kuwa na mabadiliko ambayo yataacha nchi ikiwa na umoja, amani bila mizozo yoyote. Anakumbusha kuwa hilo liliibuka kwa kuiangalia Zanzibar kuwa ilijichukuliwa madaraka.

"Tukaona hakuna sababu ya kuwanyang'anya tuiache ibaki kama ilivyo. Lakini bila ya majadiliano kwenye Bunge Maalumu wameweka kifungu kinachosema baada ya kupitishwa katiba hii Zanzibar lazima ibadili katiba yake ilingane na hii ya Muuungano."

Jaji Warioba anasema kwa mujibu wa maoni hayo baada ya kupitisha katiba hiyo kutakuwa na kipindi cha mpito ili kufanya baadhi ya mambo ikiwamo kurekebisha Katiba ya Zanzibar ili iwiane na ya Muungano.

"Huenda hilo lisiwezekane kwa sababu katika kukusanya maoni wananchi walisema ili kubadili Katiba ni lazima kupata maoni ya wananchi." Anakumbusha.

Anapendekeza katika katiba pendekezwa kifungu hicho kiondoke kwani ana wasiwasi kuwa Wazanzibari hawatakiridhia hivyo huenda katiba hiyo isikubalike.

"Nataka kiondoke kwa vile Zanzibar ni tulivu baada ya Rais Hussein Mwinyi kuwaunganisha na kuondoa tofauti zao."

Anasema Watanzania wanaweza kuamua namna bora ya kupata Katiba mpya na kurekebisha katiba pendekezwa na suala la muda wakaamua pia.

> Rais Kikwete alipohutubia Bunge Maalumu alitaja mambo hayo kuwa yameondolewa kwenye orodha ya vitu vya Muungano...

Anasema kwa sasa ni vigumu kuwa na maoni ya wananchi kwa sababu ya corona isiyoruhusu kufanya mikusanyiko.

Anasema la muhimu ni imani kwa kuwa Rais Samia amekubali kukutana na wanasiasa wenzake akifanya hivyo watazungumza na kukubaliana ni katiba ipi wanayopeleka kwa wananchi na katika kipindi gani na kwa njia gani?

Anasema hayo wanaweza kufanyika lakini kuna ambayo yalitokana na wananchi lakini mengine siyo. Kabla ya mchakato serikali mbili ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar ziliamua licha ya kwamba hayakuwapo kwenye mchakato na yakaondolewa kwenye mambo ya Muungano.

"Rais Kikwete alipohutubia Bunge Maalumu alitaja mambo hayo kuwa yameondolewa kwenye orodha ya vitu vya Muungano kuwa ni pamoja na bandari, utafiti, takwimu, mafuta na gesi. Serikali zimeyaondoa bila kubadili vipengelea kwenye katiba."

Anataka yabadilishwe kwenye katiba kwani kiliichofanyika sasa kimefanywa bila kubadilisha kwenye katiba vipengele hivyo. Anasema ni kosa kikatiba serikali zikiondoa vipengele hivyo ni lazima ziviondoe pia kwenye katiba ya sasa.

### BUNGE LINAWEZA KUIBADILI

Jaji Warioba anasema Bunge la sasa linaweza kubadilisha katiba na kuingiza mabadiliko ya wananchi wanayoyataka endepo watakubaliana.

Kwa mfano suala la kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, matokeo ya rais kupingwa mahakamani na rais kuchaguliwa na zaidi ya asilimia 50 ya wapigakura.

Anasema yalitajwa na wananchi na Tume ya Katiba ikayaingiza kwenye rasimu, hivyo wakati wanaondoa orodha ya mambo ambayo si ya Muungano wanaweza kutumia fursa hiyo kurekebisha vipengele hivyo vya kikatiba.

Anakumbusha kuwa yote yanawezekana pale Rais na wanasiasa watakapokaa pamoja kuzungumza na kufikia muafaka wa namna ya kukamilisha kuandaa katika mpya na muda utakaotumika kupata andiko hilo jipya .



# HABARI DODOMA

## Waziri Jafo akipa kiwanda siku 14

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ametoa wiki mbili kwa Kampuni ya Yapi Merkezi kufukia mabwawa ya majitaka yaliyopo eneo la Zuzu jijini Dodoma, baada ya kubainika kutozingatia matakwa kimazingira.

Jafo alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akikagua mabwawa ya kutibu majitaka katika mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwenye eneo hilo.

Alisema mabwawa hayo yamechimbwa bila kushirikisha Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

"Hamkwenda DUWASA mmeamua kufanya kazi wenyewe shughuli zenu lazima mfuate masharti ya serikali lazima mwende NEMC kwa hiyo vyote hamkufanya. Nini mpango wenu sasa? Mtu wa mazingira nataka nijiridhishe nitakuja hapa niangalie nawapa wiki mbili."

"Huu mradi ni wa kwetu wote lakini vilevile yale masharti lazima tuyafuate tusifanye huu mradi ukaleta athari kwa watu haiwezekani hapa kuna wakazi wa aina mbalimbali ukiangalia uchafu wa hapa huwezijua inawezekana watoto wa hapa wadogo wanatoroka kuja kufanya kitu tofauti," alisema.

Waziri Jafo aliwataka kujenga miradi ambayo itabaki na wananchi wataitumia hata baada ya kukamilika kwa miradi hiyo.

"Tujifunze kwanini katika kambi za wakimbizi kunajengwa shule kunajengwa vitu vingine hata wakimbizi wakiondoka miundombinu inaendelea kutumika tujifuze kwanini Tanroad wakitengeneza barabara kwanini zile nyumba zinazobaki zinatumika katika miundombinu."

"Kuna uharamu gani nyinyi mkapata mtaalamu mkatengeneza mabwawa mkimaliza hapo inakuwa sehemu ya miundombinu serikali na watu itaendelea kuitumia siku zingine," alisema.

Alimtaka mkandarasi wa kampuni hiyo kufuata matakwa ya masharti ya kimazingira ili kuwalinda wananchi.

"Nitoe maelekezo kwa makandarasi wengine wenye miradi ya kuchimba mabwawa lazima wafuatilie matakwa ya masharti ya kimazingira kwa sababu lazima tuweke miradi na lazima tuwalinde wananchi ambao tunawawekea miradi hii kiufupi hapa sikuridhika na hichi nilichokiona," alisema.

Kaimu Meneja wa NEMC, Kanda ya Kati, Emmanuel Mwasilu, alisema kabla ya Waziri Jafo kufika walifika katika mradi huo na kubaini mazingira kutoridhisha na kuipiga faini kampuni hiyo ya Sh. milioni 50 na kuwaagiza miundombinu hiyo iondolewe eneo hilo.

"Wameshasitisha, lakini wafanye uchapushaji kuwe katika hali nzuri maelekezo mengine ya Waziri tunayachukua kwa ajili ya kuwaelekeza wakandarasi wengine. Nitoe wito kwa wananchi, taasisi mbalimbali na Wakandarasi waweze kufuata sheria na maelekezo ambayo tunakuwa tumewapa katika vibali," alisema.

# Mikoa vinara ukatili wa kijinsia, watoto yatajwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limetaja mikoa mitano iliyoongoza kwa kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya miezi sita, huku likitaja sababu kadhaa ikiwamo imani za kishirikina.

Aidha, mikoa 15 imetajwa kuongoza kwenye matukio ya mauaji, ubakaji naulawiti wa watoto.

Akitoa taarifa ya hali ya usalama nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni, mwaka 2021, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camillus Wambura, alitaja takwimu za ukatili wa kijinsia kwa Mkoa wa Arusha ni 1,697, Ilala (1,486), Tanga (1,347), Kinondoni (924) na Lindi (780).

Kwa upande wa makosa ya ukatili kwa watoto, alisema takwimu za matukio ya mauaji Mkoa wa Kagera ni 11, Mwanza (9), Rukwa (4), Kilimanjaro (4) na Dodoma (3).

"Kwa ubakaji Tanga inaongoza ambapo matukio 178 yameripotiwa, Mbeya ni162, Mjini Magharibi (155), Morogoro (155) na Kilimanjaro (149)," alisema.

Kadhalika, alisema matukio ya kulawiti Mjini Magharibi inaongoza kwa matukio 66, Arusha (44), Kinondoni (49), Temeke (55) na Ilala (23).Kwa mujibu wa Wambura, sababu ya matukio hayo ni imani za kishirikina, mmomonyoko wa maadili, wivu wa mapenzi na tamaa za mwili.

"Nimewaita kuwahabarisha kuhusu kuibuka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia na waathirika wakubwa ni watoto, wanawake na vikongwe licha ya takwimu za makosa makubwa kupungua kwa asilimia 4.6 kutokamakosa 26,011 mwaka 2020 hadi 24,805 mwaka huu," alisema.

Wambura alitoa wito kwa viongozi wa dini kuelimisha waumini wao kuhusu tabia zilizoibuka za kuuawa watoto kwaimani za kishirikina.

"Aidha, wanawajibu wa kuhakikisha wanaimarisha operesheni na doria za kiimani katika nyumba za ibada kwa waumini kwa kukemea tabia za ovyo, ambazo zimeanza kuibuka katika jamii ya kitanzania," alisema.

Aliwahimiza wazazi na jamii kuwa karibu na watoto na ina jukumu la kuwatambua na kuwafichua wahalifu katika maeneo yao.

"Viongozi wa kisiasa pia wana wajibu wao kuhakikisha amani imetamalaki kwenye maeneo wanayoyaongoza, ikiwamo ulinzi wawatoto na pia kukemea na kuchukua hatua za kisheria kwa matukio yanayotokea na kuwafichua wahalifu wa matukio haya," alisema.

"Chama cha Tiba za Asili nchini nawaagiza kuwachukulia hatua kali waganga wa jadi wadanganyifu ikiwamo kuwanyang'anya leseni zao, waganga wa jadi wanaowaaminisha watu kwa kupiga ramli chonganishi kuwa watapata mali wakiua watoto...tambueni serikali haijawahi kushindwa itawatafuta popote walipo ili kukomesha tabia hii," alisema.

Aliviomba vyombo vya habari kuandaa vipindi vitakavyoelimisha jamii kuhusu kuibuka na madhara ya ukatili wa kijinsia.



Ofisa wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ), Umehani Khatri (kulia), akizungumza wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa mahesabu kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kutoka mikoa mbalimbali, yaliyofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri: Siasa isiingizwe kwenye sensa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeitaka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na wadau kutoingiza siasa katika mchakato unaondelea wa kupitia dodoso la sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti, 2022.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia walemavu, Ummy Nderiananga, alitoa kauli hiyo kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, katika kikao cha wadau cha kupitia dodoso hilo.

Alisema serikali inawetegemea hivyo wasiingize siasa kwenye dodoso hilo na badala yake wajadili kitaalamu kwa kuwa makundi yote muhimu yamejumuishwa.

Aliagiza NBS kupokea na kuyafanyia kazi mapendekezo yote yatakayotolewa na wadau kuhusiana na sensa hiyo na kwamba chanzo kikuu cha kukusanya taarifa za kitakwimu ni ngazi zote za kitawala.

Alisema asilimia 40 ya viashiria vya malengo endelevu vya dunia vya mwaka 2030 na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo vinategemea taarifa za kitakwimu kutoka katika sensa ijayo hivyo ni vyema wakatumia nafasi hiyo kuhakikisha wanapata maoni mazuri kutoka kwa wadau.

Kadhalika, alisema takwimu za sensa hiyo zitaisaidia serikali ya awamu ya sita kufuatilia na kutathmini malengo yaliyowekwa katika mipango ya maendeleo hususani mpango wa tatu wa maendeleo na dira ya taifa ya maendeleo ya mwaka 2025 kwa lengo la kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema katika dodoso hilo lina maswali 94 ambalo wananchi watatoa majibu kulingana na mwongozo ulioainishwa ikiwamo hali za ajira zao.

Alisema maswali hayo yameongezeka ikilinganisha na sensa ya mwaka 2012 ambayo ilikuwa na maswali 64 huku mwaka 2002 yalikuwa 34.

Kwa upande wake, Kamisa wa Sensa, Anne Makinda, alitoa wito kwa wadau kushiriki vyema jukumu hilo la kupitia dodoso ni kubwa na ndio sensa yenyewe.



# DC aagiza uchunguzi walioiba mabomba ya maji

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza, SACP Ismail Mlawa, ameliagiza Jeshi la Polisi, kufanya uchunguzi na kuwakamata wote waliohusika na wizi wa mabomba ya maji yaliyokuwa yatumike kwenye ujenzi wa mradi wa maji uliopo katika Kata ya Mababu.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kukagua mradi wa maji Kata ya Mababu, kuwa wizi huo ulifanyika wakati bado hajaripoti wilayani Kyela na kwamba ndani ya muda mfupi wahusika watakamatwa.

Alisema hadi sasa hakuna hatua zilizochukuliwa na viongozi wa mababu na kulazimika kuingilia kati na kuahidi kutumia mbinu za kijeshi kuwabaini wezi hao.

"Huo ni ubinafsi unaibaje mali ya umma ambayo kila mmoja atanufaika nayo, tena mradi muhimu kama huu mtu unakwamisha bahati mbaya wakati mambo hayo yanaibwa mie nilikuwa bado sijaripoti sasa ndani ya muda mfupi watuhumiwa wote watakamatwa," alisema SACP Mlawa.

Diwani Kata ya Mababu, Rashid Yahya, alisema wizi wa mabomba hayo umekwamisha shughuli za kukamilisha mradi huo na kuwaomba wananchi kutoa ushirikiano ili wahusika wachukuliwe hatua.

Alisema mradi huo umeanza kunuifaisha kijiji cha Kilombero huku vijiji vingine vikiwa bado ikiwamo cha Ngyekye ambacho kina idadi kubwa ya watu kama vile wafanyabiashara.

Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA), Wilaya ya Kyela, Mhandisi Tanu Deule, alisema jumla ya mabomba manane yaliibwa na watu wasiofahamika kwenye stoo ya kijiji.

Alisema mabomba hayo yalitosha kutandazwa kwa kilomita moja karibu na kuwafikia wananchi na wizi huo umekwamisha utandazaji hali inayowalazimu kusubiri fedha ili wakanunue mabomba mengine.

Alisema zaidi ya Sh. milioni 500 zimetumika kujenga mradi huo wa maji wa Mababu ambao utahudumia maeneo mbalimbali ikiwamo kata za Makwale na Matema.



Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza na Joyce Isack (aliyekaa kwenye kiti mwendo), mkazi wa Sinde, jijini Mbeya, ambaye alipata ajali ya gari iliyomsababishia ulemavu wa kudumu wa miguu, baada ya kumkabidhi mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba yake, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Dk. Tulia atoa mil. 500/- ujenzi kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, ametoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iyela ili kuwasaidia wananchi kukabiliana na adha ya kutembea umbali mrefu na gharama za kupata matibabu maeneo mengine.

Alitoa msaada huo jana wakati akizungumza kwenye mkutano maalum na wananchi wa Iyela uliokuwa na lengo la kuwaeleza vipaumbele vilivyowekwa na serikali katika kuwasaidia wananchi.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2021/2022 chini ya Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imejikita kuboresha miundombinu ya barabara, elimu na afya.

Kwa kutambua umuhimu huo, Dk. Tulia alisema serikali imetoa Sh. milioni 500 kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya ambacho kitakuwa msaada kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo huku akiwaeleza kuhusu uamuzi ulioyafanyika kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji ya kuanza mara moja ujenzi wa kituo hicho.

"Kwa muda mrefu wananchi wa Kata ya Iyela wamekuwa wakipata huduma za matibabu maeneo mengine, kwa kutambua adha hiyo serikali imetoa kiasi cha Sh. milioni 500 kuanza ujenzi huku tukiwahamasisha pia wananchi kushiriki nguvu kazi zao ili kituo hiki kikamilike kwa wakati," alisema Dk. Tulia.

Katika hatua nyingine Dk. Tulia alifanya ziara ya kuwatembelea baadhi ya wananchi hususani wenye mahitaji maalum akiwamo Joyce Isack, mkazi wa Sinde, ambaye alipata ajali ya gari na kumsababishia ulemavu wa kudumu.

Alimsaidia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kumwezesha kukamilisha ujenzi wa nyumba yake, vile vile alimsaidia Gabriel Mwangobola, mkazi wa Uyole baiskeli mwendo kwa ajili ya kutembelea baada ya kupata ajali miaka kadhaa iliyopita akiwa mwalimu wa Shule ya Sekondari Sangu pamoja na fedha Sh. 600,000 ili kuanzisha biashara itakayomsaidia kujikwamua kiuchumi.

Baadhi ya wananchi wa Iyela akiwamo Tukupasya Wisdom, alisema kujengwa kwa kituo hicho kutasaidia wajawazito kupata huduma karibu ikilinganishwa na ilivyokuwa awali walienda kujifungua maeneo ya mbali. Wisdom alisema kulingana na miundombinu ya eneo hilo walilazimika kubebwa kwenye pikipiki kwenda maeneo mengine kama Kituo cha Afya cha Nzovwe kujifungua.

# Watumia nguvu zao kujenga barabara km. 2

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Iwambi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wametumia nguvu zao kujenga barabara yenye urefu wa zaidi ya kilomita mbili ili kurahisisha mawasiliano ya barabara kati ya eneo lao na maeneo mengine ya jiji.

Wananchi hao wameiomba serikali iwasaidie utaalamu wa kuweka mitaro na makaravati ya kupitisha maji ili barabara hiyo idumu kwa muda mrefu huku wakisema kuwa wameijenga barabara hiyo kwa kuchangishana fedha kwa ajili ya kukodi mitambo.

Wakizungumza na Nipashe jana wananchi hao walisema waliamua kujenga barabara hiyo baada ya kuona wanapata shida ya kusafiri kutoka katika eneo hilo kuunganisha katika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Charles Mtagwaba, ambaye ni miongoni mwa wakazi wa eneo hilo, alisema awali katika eneo hilo hapakuwa na barabara isipokuwa palikuwa na wigo uliokuwa unatenganisha shamba la mifugo na maeneo ya wananchi.

Alisema baada ya wananchi kuongezeka katika eneo hilo waliamua kuanza kulima barabara hiyo kwa kutumia jembe la mkono, lakini walikuwa wanashindwa kufanikiwa kwa sababu mafuriko yalikuwa yanazoa udongo na kusababisha makorongo.

"Baadhi ya watu huku sasa hivi wana magari, lakini sasa barabara imeharibika, mafuriko yalisababisha makorongo mengi sasa tumeona ni vema tuchangishane ili kuiboresha, sasa sisi tumeijenga lakini tunahitaji utaalamu kutoka serikalini ili mitaro iwe ya kisasa," alisema Mtagwaba.

Naye John Chigazi, alisema wamejenga barabara hiyo kwa kiwango cha kawaida na wanaiomba serikali iwasaidie kuboresha zaidi ikiwa ni pamoja na kuweka vifusi vyenye ubora na mitaro imara kwa maelezo kuwa wao hawana utaalamu.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kuunganisha makazi yao na barabara kuu ambayo inawaunganisha na eneo la katikati ya Jiji la Mbeya ambako ndiko huduma nyingi muhimu zinapatikana.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Jiji la Mbeya, Mhandisi Seleman Mziray, alisema barabara hiyo kwenye mtandao wa barabara na wakala huo na hivyo akawataka wananchi hao kuendelea kufuata taratibu.

Alisema wananchi hao wanatakiwa wafuate taratibu za kuomba ili barabara hiyo ianze kuhudumiwa na TARURA huku akiwapongeza wananchi hao kwa kuamua kuijenga.

Alisema wananchi hao wanatakiwa kuanza mchakato wa kuomba barabara hiyo kwa kuanza na mikutano ya mitaa yao kisha wawasilishe mihutasari yao kwenye Kata kabla ya kufikishwa kwenye vikao vya halmashauri.

"Sisi tukishafikishiwa taarifa hizi tunaenda kuitembelea barabara husika na kuamua kuanza kuisimamia, lakini sisi huwa tunaletewa fedha kwa ajili ya kuhudumia barabara ambazo zipo kwenye mtandao tu," alisema Mziray.





# Umuhimu wa sensa wabainishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Sada Mkuya, amesema sensa ya watu na makazi inasaidia kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kutunga sera na kupanga mipango ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau waliokuwea wakijadili dodoso la sensa la mwaka 2020/2022 Mjini Zanzibar.

Alisema matumizi ya takwimu ni muhimu sana katika mipango ya serikali, ndio maana nchi imekuwa ikifanya sensa kwa muda uliopangwa bila ya kukosa, kutokana na umuhimu wake.

Alisema serikali itahakikisha zoezi hilo linafanyika kwa ufanisi, na kwamba sensa ya mwaka 2022 ni tofauti ukilingnaisha na zilizopita.

Alieleza kuwa upatik anaji wa takwimu zinatazotokana na sensa zitatumika kupima mafanikio ya dira na mipango ya maendeleo.

"Tunawashukuru wadau wa maendeleo kwa kuendelea kushirikiana na serikali kutusaidia kuona kwamba hili zoezi ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa maendeleo," alisema Dk. Mkuya.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mayasa Mahfoudh, alisema wameamua kujadili dodoso la sensa ili kufanya maandalizi mapema, na kwamba sensa ya mwaka 2022 itakua ni kipekee.

"Sensa ya 2022 itakuwa ni ya kipekee kwa sababu ni ya kidigitali itakayowezesha kupata matokeo kwa muda mfupi na kupunguza gharama," alisema.

Alisema sensa hiyo kwa mara ya kwanza itawezesha kupata takwimu na viashiria mbalimbali vya kiuchumi na kijamii hadi ngazi ya shehia kulinganisha na iliyopita, ambayo iliruhusu kutoa takwimu katika ngazi za wilaya.

Aliongeza: "Sensa ni takwa la kisheria na inafanyika kwa kufuata mpango maalum, hivyo hadi sasa mbali ya hatua ya kujadili, tunaendelea kukamilisha miongozo mbalimbali ya kusadia watu, alisema na kuendelea:

"Maandalizi mengine ni kufanya majaribio mwaka huu, kutoa mafunzo kwa watumishi mbalimbali wakiwamo wadadisi na wasimamizi."

Aidha, alisema madodoso yaliyojadiliwa katika mkutano huo yataweza kuwapatia taarifa za kupata viashiria vya hali ya kidemokrasia na kijamii kama umri, hali ya ulemavu, elimu, afya, uhamaji, vizazi na vifo, makaazi, kilimo, misitu, uvuvi na utunzaji wa mazingira ambapo taarifa hizo zitatumiwa na wadau mbalimbali.

## Bidhaa zinazodaiwa za magendo mbaroni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kimekamata watu watano kwa tuhuma za kusafirisha bidhaa kwa njia ya magendo.

Mkuu wa doria wa kikosi hicho Kamandi ya Kusini, Luteni Mahmoud Muhsin, alisema askari wakiwa katika doria za kawaida walikamata mashua iitwayo 'Mwanzo Mgumu' ikiwa na watu watano wakiwa na sukari viroba 70, runinga bapa sita, jokofu mbili, draya 11 na baiskeli moja, wakielekea Kunduchi, mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza jana eneo la tukio huko Kizimkazi, alisema kusafirisha bidhaa kinyume cha sheria ni kuikosesha mapato serikali, hivyo aliwataka wananchi kutii sheria za nchi bila ya kushurutishwa.

Naye Kaimu Kamanda wa kamandi hiyo, Hassan Hussein Ali, aliwataja watuhumiwa hao waliokamatwa na bidhaa hizo ni Burhan Mwinyihaji (30), Abdallah Mwinyi (25), Ismail Kudura (35), Juma Kiboga (45) na Ali Pandu (30), wote wakazi wa Uzi Kisiwani Unguja.

Aliwataka wananchi wa Zanzibar kuacha kusafirisha bidhaa kwa njia zisizokubalika, na kwamba serikali na kufanya hivyo ni kosa kishearia.

"Kusafirisha bidhaa zozote bila ya kibali ni kosa kisheria, niwatake wananchi hasa wavuvi kuacha kubeba jukumu la kupokea bidhaa ambazo hazina vibali vyoyote kutoka eneo moja kwenda linguine," alisema.

Anas Omar Anas, Mkuu wa kitengo cha majahazi kutoka Mamlaka ya Usafiri Baharini, aliipongeza KMKM kwa ushirikiano wa karibu na mamlaka hiyo, na kuwataka wananchi wanaojihusisha na biashara kwa njia ya magendo kuacha kwa kuwa serikali iko macho katika kupambana na magendo na uhujumu uchumi.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (wa pili kulia), akipokea msaada wa vitabu mbalimbali vya sayansi na hisabati kutoka Shule ya Sekondari ya Lancley Academy ya Berkshire nchini Uingereza, kwa ajili ya wanafunzi wa shule za Zanzibar jana. Wapili kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya shule hiyo, Prof. Hamed Rashid Hikimany. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Zanzibar yapigwa jeki vitabu shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema mataifa mbalimbali yapo tayari kuisaidia Zanzibar kimaendeleo ili izidi kupiga hatua ya kufikia malengo ya uchumi wa buluu hasa katika sekta ya elimu.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya kukabidhiwa vitabu vya Sayansi Mjini Unguja kutoka Shule ya Sekondari ya Langley Academy iliopo mtaa wa Be rkshire nchini Uingereza.

Alisema nchi yeyote ili ifikie malengo, ni lazima iwe na misingi imara ya elimu ambayo ndio ufunguo wa maisha.

Aidha, alieleza kuwa Zanzibar ipo tayari kutoa ushirikiano na nchi mbalimbali, lengo ni kuendana na kasi ya maendeleo ya uchumi wa buluu.

Aidha, aliwaomba Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kuhakikisha wanaisaidia Zanzibar katika nyanja zote za maendeleo.

Alisema vitabu hivyo watagawiwa katika Shule zenye uhaba kwa sababu kuna baadhi ya wanafunzi wanatumia kitabu kimoja watu wawili. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa shule hiyo, Prof. Hamad Rashid Hikimany, alisema wametoa vitabu ili kuunga mkono masomo mbalimbali hasa ya sayansi, hatua ambayo itasaidia wanafunzi kufaulu vyema.

Aidha, alisema malengo yao ni kuhakikisha wanatoa misaada katika kuleta maendeleo ya taifa lao hasa sekta ya elimu, na kwamba vitabu vya dini zote vimetilia mkazo suala la elimu.

Zaidi ya vitabu 1,000 kutoka shule hiyo, vilikabidhiwa vikiwamo vya Hesabati, Kemia, Fizikia na Kingereza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.206/2021**

Ombi la **PILLI ABDUL NGOWO** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **ABDUL ALLY NGOWO**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 17/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 12/07/2021**

MOROGORO

116354622

## CHETI KIMEPOTEA



**EMILIANA LUCAS MAHUNDI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.4624/0008** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA **PREMIER GIRLS** SECONDARY SCHOOL MWAKA **2018.** YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/KIL/RB/337219/2021.**

116356802

## CHETI KIMEPOTEA



**WILLIUM KONDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P0203/0601/2016** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka **2016** katika kituo cha shule ya Sekondari Iringa Girls. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi:
**IRI/IRI/RB/663832/2020**

116356702

## KUPOTEA KWA VYETI



**ELISHA O ASSERI** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo, cha kidato cha nne chenye index namba **S 1198-0047** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya TANZANIA ADVENTIST mwaka 2009, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S 0818-0559** kilichotolewa na shule ya secondary ya TARAKEA mwaka 2012, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **KIL/MOS/RB/718563/2020**

116356402

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Ujamaa Community Resource Team
PO Box 15111, Arusha, Tanzania
www.ujamaa-crt.org

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI.

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MIRADI MIPYA IPATAYO MITANO KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA JULAI 2021 MPAKA 2022

1. UCRT KWA KUSHIRIKIANA NA OXFAM TANZANIA LITATEKELEZA MRADI WA "USAWA WA KIJINSIA NA UWEZESHWAJI KIUCHUMI KWA WANAWAKE NA VIJANA" WILAYANI HANANG' KATIKA VIJIJI VYA MURERU, DIRMA, KINYAMBURI, GASABOY, MING`ENYI DAWAR, GAWIDU NA MUUNGANO UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI **115,044,426.00**
2. UCRT KWA UFADHILI WA MALIASILI INITIATIVE ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA ``ADVANCING LAND RIGHTS OF PASTORAL WOMEN IN NORTHERN TANZANIA `` KATIKA WILAYA YA SIMANJIRO NA MONDULI UTAKAOGHARIMU KIASI CHA DOLA ZA KIMAREKANI **$ 155,000**
3. UCRT KWA UFADHILI WA LINCOLN PARK ZOO ("LPZ") ITATEKELEZA MRADI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI KWA VIJIJI VYA SUKURO, KITIANGARE WILAYA YA SIMANJIRO NA KIJIJI CHA ELUWAI WILAYA YA MONDULI UTAKAOGHARIMU DOLA ZA KIMAREKANI **$27,0000**

***MIRADI HII YOTE ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.***

116357302

**KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tz na manager@ujamaa-crt.or.tz**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB:
+255 - 0782253676

Uza, Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie
0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# W'biashara K'koo kuhamia Kisutu, Machinga Complex

**Na Maulid Mmbaga**

WAFANYABIASHARA wa Soko la Kariakoo sasa watahamishiwa katika masoko ya Kisutu na Machinga Complex, Ilala ili kupisha uchunguzi na ukarabati wa soko lililoungua.

Akizungumza jana wakati alipotembelea soko hilo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliwashukuru wafanyabiashara hao na kuwaahidi kuwa ataratibu suala la kuhamia katika masoko hayo mengine kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao.

Alisema kitendo cha wafanyabiashara hao kukubali kuhama kwa muda kitasaidia suala la uchunguzi na ukarabati kufanyika kwa weledi, huku akiwataka kuhakikisha kuwa taarifa zao zimeratibiwa kabla ya kuondoka ili watakapokwenda katika masoko hayo mengine wasilipe kodi kwa muda wa miezi miwili.

"Nia ya serikali sio kuwaondoa wafanyabiashara ila ni kuwasaidia Watanzania walioathirika, kama walikuwa wanapata ridhiki hapa ni wapi kwingine wanaweza wakapatia wakati jambo hili linaendelea kushughulikiwa huo ndio mtazamo wa serikali.

"Hatuna nia ya kumkomoa mtu yeyote zaidi kipindi hiki tunatakiwa kushikamana na mimi nimesema wazi mtu atakayeratibiwa kutoka Soko la Kariakoo wenye maduka yanayoitwa vigori walikuwa ghorofa ya kwanza, pili, akapelekwa soko lingine mambo yatakapokamilika hao tunawapa kipaumbele kurudi hapa," alisema.

Aliongeza kuwa hiyo ndiyo nia ya serikali kuliko kukaa hapo na kuanza kulumbana kwa kuwa hakuna kitakachoendelea zaidi ya kucheleweshana kupata ridhiki.

"Mimi niwaombe lililojitokeza hapa la mvutano ambalo mnasema sisi bora tuondoke wote, sisi tumepita tumeangalia soko si kwamba tunataka kuwagawa tumepita tumeongea na wenzangu kwamba kweli hapa leo leo tulete wataalamu wengine kama soko litakarabatiwa likarabatiwe lote," alisema.

Aidha, wakati huo wataleta wataalamu wafanye tathmini, lakini hilo halitokwamisha utaratibu waliouweka wa kuondoka, na alisema kuwa ana takwimu za kutosha, nafasi za maduka zilizopo Machinga na Kisutu na akisikia kuwa kuna aliyekosa nafasi, atampeleka popote patakapopatikana.

Pia, aliwasisitiza kutowazingatia wapotoshaji wanaosema kuwa wakiondoka katika soko hilo hawatorudi na aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa soko likikamilika watapewa kipaumbele kurudi kama walivyoondoka ndivyo watakavyorudi.

Kuhusu wafanyabiashara soko dogo, Makalla alisema biashara ziendelee, lakini tayari ametuma timu ya wataalamu wa ujenzi kwa ajili ya kufanya tathmini endapo soko kubwa litakarabatiwa na kukaonekana umuhimu nalo lifanyiwe ukarabati hapo baadaye.

Alisema kwa wakati huu wafanyabiashara wa soko dogo wataendelea na biashara zao kama kawaida huku akisisitiza agizo la kutaka barabara za kuingia sokoni hapo kuachwa wazi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Tume ya Uchanguzi Zanzibar, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri atoa maelekezo 12 Bodi TASAC

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, ametoa maelekezo 12 kwa bodi na menejimenti ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC).

Miongoni mwa maagizo hayo ni kuzingatia matumizi sahihi ya fedha na kufuata taratibu za vikao kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Pia ameitaka bodi hiyo kujiepusha na makosa yote yaliyojitokeza kwenye bodi iliyopita, ikiwamo kuwa na idadi kubwa ya vikao na matumizi, ambayo yalimshutua Rais Samia Suluhu Hassan na kwamba wakienda kinyume hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa TASAC, Dar es Salaam, Dk. Chamuriho alisema bodi hiyo ina mchanganyiko wa wajumbe wapya, wa zamani na kutoka sekta binafsi, hivyo imezingatia uwakilishi sahihi katika sekta ya usafirishaji majini ambao wanatarajiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia weledi, maelewano, umahiri mkubwa na ufanisi wa hali ya juu.

Waziri Chamuriho alitaja ya kuzingatia kuwa ni nyaraka na miongozo inayotolewa na msajili wa hazina, muundo wa utumizi unajazwa na unatekelezwa kikamilifu, uwapo na utekelezaji mikataba ya utendaji (Bodi, Msajili wa Hazina, Mkurugenzi Mkuu na Katibu Mkuu (Uchukuzi).

Mengine ni kuandaa programu/ratiba ya shughuli za bodi kila mwaka na kuzisimamia (mikutano, ziara na mafunzo), kuandaa mikutano ya Bodi na Kamati kwa kila robo mwaka na kupitisha taarifa za utendaji ili zifikishwe kwenye mamlaka na wizara, kuzingatia sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake katika manunuzi yote na kuondoa samani, nyaraka na vifaa vingine vya shirika. Maagizo mengine ni kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa bila upendeleo kwa watoa huduma na wateja kwa ujumla, kuhakikisha hakuna mgongano wa kimaslahi au sheria na taasisi zingine za serikali katika uetekelezaji wa majukumu ya shirika, kushirikisha wadau na watoa elimu kwa umma kuhusu shughuli na majukumu ya shirika.

Pia kushughulikia kikamilifu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na zilizotolewa na ukaguzi wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), kuongeza ushirikiano na Zanzibar, kusimamia ukusanyanji mapato na matumizi yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za shirika ikiwamo kuwasilisha mchango wa TASAC Hazina.

"Naiagiza Bodi kuzifanyia kazi haraka iwezekanavyo changamoto za kiutendaji hususan zinazohusu majukumu ya kibiashara, ili kuwahakikishia wateja wenu huduma bora na wenye gharama nafuu. Kwa changamoto za kisheria ninawaagiza kuzifanyia kazi kwa kushirikiana na wadau na kuwasilisha maoni yenu wizarani ili zile zinazohusu Bunge kufikishwa kwenye mhimili huo kwa mujibu wa taratibu zilizopo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TASAC, Kapteni Musa Mandia, alimhakikishia Waziri kuwa bodi itazingatia na kutekeleza majukumu yake kwa uaminifu na waledi mkubwa kwa kuwa lengo ni kwenda mbali na siyo kwenda haraka, na kwamba watahakikisha wanarekebisha upungufu uliopo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Kaimu Mkeyenge, alisema aliiomba bodi itakapoanza kazi kushughulikia suala la wanaokaimu, hoja iliyoungwa mkono na waziri na kuagiza wakurugenzi watano wanaokaimu wapewe nafasi hizo au wakamilishe kwa kufuata taratibu ili kuharakisha utendaji kazi mzuri.

***Imeandikwa na Salome Kitomari na Christina Mwakangale***

# Waliotozwa fedha kwa ujauzito warejeshewe

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amelaani vikali kitendo cha wazazi kutozwa faini ya Sh. 245,000 na mifuko 10 ya saruji baada ya watoto wao kupata ujauzito wakiwa shuleni mkoani Mbeya.

Kadhalika, ameagiza fedha hizo zilizokusanywa kurudishwa kwa wazazi kwa kuwa kitendo hicho ni kinyume cha utaratibu wa elimu nchini na faini hizo haziwezi kuondoa tatizo la wanafunzi kupewa mimba.

Akizungumza juzi kwenye mkutano wa shina Kata ya Kandete, Busekelo mkoani humo, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, kusitisha utekelezaji wa uamuzi wa bodi za shule na kurejeshwa kwa fedha zote zilizokusanywa kama faini kwa waliowapa na waliopokea (wanafunzi) wa shule za sekondari na msingi.

Shaka alisema ni jambo la ajabu kwa halmashauri hiyo kujiwekea utaratibu wa kuwatoza faini wazazi ambao watoto wao ni watoro au wamepata ujauzito.

"Hatuwezi kukomesha vitendo vya kuwapa mimba watoto wetu wa kike kwa kuendelea kutozana faini kwa wazazi wote, yaani mtu mwanawe anapewa mimba na pesa anatozwa Sh. 245,000 na mifuko 10 ya saruji pamoja na mtenda kosa hilo halafu wote wanarejea kwenye jamii," alisema Shaka.

Aliweka bayana kuwa jambo hilo ni kinyume cha Sheria ya Elimu na kwa namna yoyote haiwezekani kwa waliopewa dhamana ya kuisimamia na kutafsiri sheria kubadilisha maudhui na kutafsiri wanavyotaka wenyewe.

"Mkuu wa Wilaya sitisha utekelezaji wa uamuzi huu kwa shule zote, na fedha zote zilizokusanywa zirejeshwe kwa wahusika na hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zichukuliwe kwa waliohusika na tupewe mrejesho ndani ya siku saba," alisema Shaka.

Alisema CCM imesikitishwa na ongezeko la matatizo ya ujauzito na utoro uliokithiri kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe tabia ambayo inachangiwa na vitendo vya rushwa na urasimu uliokithiri.

Pia alisema rushwa na urasimu ni vitendo na tabia ambazo hazitavumiliwa hata kidogo na CCM na serikali zake katika kuwaletea maendeleo endelevu wananchi hatutakubali kuona baadhi ya watumishi, watendaji na viongozi waliokosa uadilifu wanawagombanisha na wananchi.




# BELLERIN atamani kwenda Milan

**MILAN, Italia**

MLINZI Hector Bellerin ameripotiwa kuwa amewaambia mabosi wa Arsenal anatamani kwenda kukipiga kwa mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Inter Milan.

Japo hakuna dili rasmi lililopelekwa Arsenal na Inter Milan kuhusu kuhitaji saini ya mchezaji huyo.

Lakini ukweli kuwa Bellerin ni moja ya majina yaliyotajwa katika shabaha za Inter Milan kufuatia kuondoka kwa Achraf Hakimi kwenda PSG kwa dau la Euro milioni 60.

Washika bunduki hao wa London wapo tayari kuachana na nyota huyo ambaye anacheza beki ya kulia hata kwa mkopo kwa sharti la kuuzwa moja kwa moja kutokana na uchezaji wake.

Bellerin alijiunga na Arsenal akitokea akademi ya Barcelona mnamo mwaka 2011 na mpaka sasa amecheza mechi 239 na kujishindia mataji matatu ya FA na makombe matatu ya ngao ya jamii.

# Nacho kubakia Madrid hadi 2023

**MADRID, Hispania**

BAADA ya klabu ya PSG kutangaza usajili wa Sergio Ramos, Real Madrid wametangaza kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba wa Nacho.

Madrid ipo kwenye sintofahamu kuhusu hatima ya baadhi ya wachezaji ambao wanataka kuondoka hapo kwenye dimba la Santiago Barnabeu.

Walishindwa kufikia muafaka na Ramos, hatimaye aliondoka kama mchezaji huru na kujiunga na PSG.

Bado hatima ya Rafael Varane pia haijajulikana na anahusishwa na Manchester United ambao wameonyesha nia kubwa ya kumtaka.


Kuongeza mkataba wa Nacho pengine ni namna nzuri ya kuboresha kikosi kutokana na ukata unaoikumba klabu hiyo ambayo mpaka sasa imemsajili David Alaba pekee.




# Maddison atarajiwa kuikamua Arsenal

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal italazimika kutoa pauni milioni 60 ikiwa wanataka kumsajili James Maddison kutoka Leicester City msimu huu wa joto.




Washika bunduki hao wanatafuta mbadala wa Martin Odegaard kufuatia uthibitisho wake kwamba hatarudi Kaskazini mwa London, na walishindwa na Aston Villa kwenye kinyang'anyiro cha saini ya Emiliano Buendia.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kocha Mikel Arteta amelazimika kumtafuta nyota mwingine katika jitihada zake za kuongeza nguvu, na Arsenal wamepewa nafasi ya kurudisha nia yao kwa Maddison.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Footbal London, ni kwamba Leicester inataka ada kubwa ya pauni milioni 60 ili kuweza kumuachia Muingereza huyo, ambaye mkataba wake bado umebakia miaka mitatu kumalizika.

Kikosi cha Maddison kinatarajia kupata ofa kutoka Arsenal katika siku zijazo, ingawa na Chelsea pia wametajwa kumvutiwa na mchezaji huyo wa miaka 24.

Mchezaji huyo wa zamani wa Norwich City alichangia mabao 15 (mabao nane, asisti saba) kwenye michezo 31 ya Ligi Kuu msimu uliopita na pia alitwaa medali ya washindi wa Kombe la FA.

# Bayern wamtaka Chiesa

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann ameonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Federico Chiesa, kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya habari vya Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alikuwa kwenye majukumu ya kitaifa na timu ya taifa ya Italia kwenye Euro 2020, na kuonekana vyema kwenye fainali ya Jumapili dhidi ya England pale Wembley.

Chiesa alifunga mabao mawili dhidi ya Austria na Hispania wakati wa hatua ya mtoano ya Euro 2020.

Kwa mujibu wa chanzo kimoja cha habari cha Ujerumani, Nagelsmann angependa kupata saini ya Chiesa, lakini amekiri fedha zinaweza kuwa tatizo.

Nyota huyo bado yupo kwa mkopo huko Juve kutoka Fiorentina, lakini ana kifungu cha kumnunua majira ya joto mwakani kwa ada ambayo inaweza kuongezeka hadi euro milioni 50.

Msimu wa kwanza wa Chiesa huko Juventus ulimshuhudia akifunga mabao 14 na asisti 10 katika mechi 43 za mashindano yote, pamoja na mechi 16 kutoka michezo 30 ya Serie A.




# MARSEILLE
## yatangaza kumwania Coutinho

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Barcelona, Philippe Coutinho yupo kwenye rada za kusajiliwa na klabu ya Marseille ya Ufaransa.

Coutinho amewekwa sokoni na Blaugrana hao na timu hiyo ya Ligue 1 imevutiwa na Mbrazili huyo.

Hali ya kiuchumi ya Barcelona ni moja ya sababu ambayo inawafanya iwauze baadhi ya wachezaji wake kwa ajili ya kupunguza gharama kubwa za kuwalipa mishahara.

Coutinho msimu mmoja uliopita alicheza kwa mkopo kule Bayern Munich ambao hawakuwa nia ya kumsajili moja kwa moja.

Hata hivyo, licha ya Barcelona kumnunua Coutinho kwa bei kubwa wakati akitoka Liverpool, wanaweza kupata hasara kwa kulazimika kumuuza kwa bei ndogo.




# Southgate: Mapema kujua hatima yangu

**LONDON, England**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate amedai kuwa ni mapema sana kuzungumzia hatima yake baada ya kufungwa katika fainali ya Euro 2020 na Italia.

Katika mechi iliyoshuhudia Italia walio kwenye moto wa kushambulia na kutawala sana eneo la kati, kocha Southgate alionekana kuishiwa ujanja na kushuhudia vijana wake wakikosa ubingwa kwenye hatua ya matuta.

Akizungumza na waandishi wa habari, Gareth alidai michuano ya Euro 2020 imekuwa chachu kubwa ya kuunganisha Uingereza na anahisi kama timu kwa pamoja wamefanya vitu vingi sana toka achukue timu hiyo mwaka 2017.

Alipoulizwa kuhusu hatima yake, Southgate alidai kuwa anatamani akapumzike na angalie marejeo na kutathmini mechi zote za michuano hii ili arudi imara kuelekea kwenye fainali za Kombe la Dunia mwakani pale Qatar.

Licha ya hilo, Gareth alikubali kubeba mzigo wa lawama wa wachezaji wake kufuatia baadhi ya vijana wadogo, ambao walikosa penalti kwa ukweli kuwa yeye ndiye aliyechagua watakaopiga.



## KWA UFUPI

### VARANE SAFI UNITED

KLABU ya Manchester United wako mbioni kukubaliana masharti binafsi na mlinzi wa Real Madrid, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akitolewa macho kwa muda mrefu.***(Daily Mail)***

### BELLERIN AITAKA INTER

HECTOR Bellerin ameiambia Arsenal kuwa anataka kuondoka wakati wa dirisha la usajili majira ya joto. Mchezaji huyo wa nafasi ya ulinzi mwenye umri miaka 26, ambaye ni mchezaji wa muda mrefu wa kikosi cha kwanza cha Mikel Arteta ana matumaini ya kuhamia Inter Milan. ***(Metro)***

### GRIEZMANN HATAKIWI

KLABU ya Manchester City haina mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30, lakini wana nia na mshambuliaji wa Norway na Borussia Dotmund, Erling Braut Haaland (20) na nahodha wa Tottenham England, Harry Kane. ***(The Sun)***

### GRIEZMANN, NIGUEL KUPISHANA

ANTONE Griezmann mwenye umri wa miaka 30 anaweza kuelekea kwenye klabu yake ya zamani ya Atletico Madrid, kwa kubadilishana na kiungo wa kati wa Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26. ***(Daily Express)***

### ISCO NJIA MOJA

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Isco amedokeza kwamba ataondoka wakati wa miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake, huku Arsenal, Tottenham Hotspur na Napoli wakimtolea macho. ***(Daily Mirror)***

### CITY, WOLVES VITANI

KLABU ya Manchester City na Wolverhampton Wanderers zote ziko katika mipango ya kumnasa mlinzi wa Fulham mwenye umri wa miaka 23, Antonee Robinson.***(Daily Mirror)***

### JESUS ANUKIA JUVE

JUVENTUS wanamlenga mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24. ***(Tuttosport, via Daily Mail)***

### ARSENAL YAMFUATA AOUAR

ARSENAL inaelekea ukingoni kumnasa kiungo mchezeshaji wa Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 23. ***(The Sun)***

### VIEIRA AMTAKA MATTHEWS

KOCHA mpya wa Crystal Palace, Patrick Vieira anampango wa kumsajili golikipa, Remi Matthews mwenye umri wa miaka 27, ambaye ameachiwa na Sunderland. ***(Daily Mirror)***



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKAJAER AJITOKEZA KUMTULIZA RASHFORD

●●●Kocha huyo asema tukio hilo litaendelea kumwiimarisha mshambuliaji wake ambaye aliivusha...

**LONDON, ENGLAND**

WAKATI Marcus Rashford, Jadon Sancho na Bukayo Saka wakiendelea kuandamwa mitandaoni, Ole Gunnar Solskjaer yupo bega kwa bega na mchezaji wake.

Suala la kukosa penalti kwenye fainali ya Euro 2020, limewaweka wachezaji hao kwenye wakati mgumu katika mitandao ya kijamii, maneno na vitendo vya kibaguzi vimekuwa vingi dhidi yao.

Mamlaka mbalimbali zimekuwa zikitoa matamko ya kukemea vitendo vya kibaguzi kwenye michezo, wachezaji na makocha mbalimbali wamezungumza kuhusu vitendo hivyo.

Na Solskjaer anaamini Rashford hatoathirika kwa kukosa penalti kwenye fainali ya Euro 2020, badala yake ataendelea kujiamini na kuongeza juhudi za kupambana zaidi hasa atakaporejea kwenye klabu yake Manchester United.

Kama ni maumivu, Rashford ameyapata kwenye fainali mbili mwaka huu, United walikosa ubingwa wa Ligi ya Europa dhidi ya Villareal na England wamekosa ubingwa wa Euro 2020 dhidi ya Italia, matokeo ya michezo yote yameamuliwa kwa mikwaju ya penalti.

Penalti ya Rashford dakika ya 93 dhidi ya PSG, iliwavusha United kucheza robo fainali ya Uefa, 2019.

"Ni suala la kawaida kupata au kukosa penalti, lakini mambo yalikuwa tofauti kwao," alisema Solskjaer akinukuliwa na Daily Mail.

"Nategemea kumwona Rashford akipambana na Fernandez na wachezaji wengine wa United kwenye kupiga mikwaju ya penalti, hivyo sina wasiwasi na hili.

# SIMBA SC KUKABIDHIWA KOMBE, MEDALI JUMAPILI

**Na Saada Akida**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imetangaza itawakabidhi mabingwa wapya wa Ligi Kuu Bara msimu huu, timu ya Simba kikombe chao baada ya mechi dhidi ya Namugo FC itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi jana inasema Simba ndio mabingwa rasmi wa msimu 2020/21 baada ya Jumapili iliyopita kufikisha pointi 79 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine licha ya kubakiwa na raundi mbili za mwisho.

TPLB katika taarifa yake ilisema inapongeza Simba kwa kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ikiwa ni kwa msimu wa nne mfululizo.

"Baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union, Simba imefikisha pointi 79 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine katika msimu huu, hivyo Julai 18, 2021 ndio itakuwa siku ya kukabidhi rasmi kombe la ubingwa wa Ligi Kuu ya Vodacom 2020/21 kwa klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam," ilisema sehemu ya taarifa ya bodi hiyo.

Bodi hiyo pia inazipongeza timu zote zilizoshiriki ligi hiyo kwa kuendelea kuonyesha ushindani wa hali ya juu ambao umesaidia kuongeza ubora na kuifanya Ligi Kuu Tanzania Bara kushika nafasi ya nane barani Afrika.

Kutokana na mafanikio ambayo Simba ilifikia katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, Tanzania Bara sasa itawakilishwa na timu nne kwenye michuano ya CAF na tayari nafasi moja ni ya wafalme hao wa Ligi Kuu.

Vita sasa imebakia katika nafasi ya pili ambayo inawaniwa na Yanga yenye pointi 70 pamoja na Azam FC yenye pointi 64 wakati Mwadui FC ya mkoani Shinyanga yenye pointi 19 imeshashuka daraja.

Pia timu za Biashara United kutoka Musoma, Mara yenye pointi 49 na Namungo ya mkoani Lindi zenyewe zinawania kumaliza msimu katika nafasi ya nne na huenda mojawapo ikapata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa kwa sababu ya ongezeko la timu lililotangazwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Timu nyingine zinazoshiriki ligi hiyo ambazo ziko katika hatari ya kushuka daraja ni pamoja na Coastal Union ya jijini Tanga yenye pointi 34 sawa na Gwambina FC (Misungwi, Mwanza) na Ihefu FC iliyopanda daraja msimu huu yenye makazi yake Mbarali, Mbeya.

Pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara litafungwa

Jumapili kwa timu zote kushuka dimbani kusaka pointi muhimu lakini msimu utafungwa rasmi kwa mechi ya fainali ya Kombe la FA kati ya mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Simba dhidi ya Yanga utakaochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.



Washiriki wa Kozi ya Mpira wa Miguu ya CAF Diploma C wakifuatilia mafunzo yanayoendelea katika ukumbi wa Chuo cha Ualimu cha Capital ulioko jijini Dodoma. Kozi hiyo ni ya miezi mitatu na inashirikisha makocha kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini. **PICHA: TFF**

# CAF yasogeza michuano ya wanawake

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF) limetangaza kusogeza mbele ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake ambayo kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) ilitarajiwa kufanyika kuanzia Jumamosi Julai 17 hadi Agosti Mosi, mwaka huu jijini Nairobi, Kenya imefahamika.

Tanzania Bara ilikuwa inawakilishwa na mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake, Simba Queens wakati New Generation Queens ilitarajiwa kupeperusha bendera ya Zanzibar.

Hata hivyo, CAF haijaweka wazi sababu iliyopelekea kusogeza mashindano hayo ambayo yalikuwa yanafanyika kwa mara ya kwanza barani Afrika.

Uamuzi huo wa CAF umekuja siku mbili baada ya Shirikisho la Soka Rwanda (FERWAFA), kutangaza timu zake mbili (vijana chini ya umri wa miaka 23 (U-23) na klabu ya Scandinavia) hazitashiriki michuano ya CECAFA mwaka huu kwa sababu ya kujikinga na ugonjwa wa corona ambayo umerejea kwa kasi.

Simba Queens ilipangwa Kundi A pamoja na timu za Lady Doves ya Uganda na PVP ya Burundi huku Kundi B likiwakilishwa na timu ya Benki ya Ethiopia, Yel Joint Stars ya Sudan Kusini na New Generation huku Kundi C likiwa na Scandinavian, FAD Club ya Djibouti na Vihiga ya Kenya.

Fainali za michuano zilitarajiwa kufanyika nchini Misri kwa kushirikisha timu nane ambazo ni vinara wa kila kundi.

## Azam yamweka sokoni Yakubu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwapo kwa tetesi za beki wake wa kati, Yakubu Mohamed kutakiwa na Yanga, mabosi wa Azam wamesema hawajapokea ofa yoyote kutoka ndani na nje ya Tanzania ambayo inamhitaji mchezaji huyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' aliliambia gazeti hili wanasikia na kusoma kwenye mitandao ya kijamii kuwa Yanga inamhitaji mchezaji huyo, lakini akaonya bado wana mkataba nyota huyo.

"Kwanza sisi hatufuati sana habari za mitandaoni, na Yanga bado hawajatuma ofa yoyote kwetu. Yakubu bado ni mchezaji wetu na ana mkataba, japo si mrefu sana, lakini hao wanaomhitaji au klabu yoyote kama inataka huduma yake tunawakaribisha tufanye biashara," alisema Popat.

Kiongozi huyo alipinga dhana Azam huwa inaikatalia Yanga inapotaka wachezaji kutoka kwao, akidai walishafanya biashara na Yanga kwa Gadiel Michael na Ditram Nchimbi.

Yakubu ambaye ni raia wa Ghana, na amekuwa akiitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya nchi hiyo, ingawa kwa sasa amekuwa hapati nafasi ya kucheza kwenye klabu ya Azam, haswa baada ya kuja kwa kocha Mzambia George Lwandamina.

## Wasanii Tanzania kukabidhiwa tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

WASANII tisa wa hapa nchini wanatarajia kupokea tuzo kwa kuvunja rekodi ya kuwa na wasikilizaji wengi kupitia App ya Boomplay.

Tuzo hizo maarufu 'Boomplay Plaques' hutolewa mara moja kila mwaka ili kutambua jitihada za wasanii wanaofanya vizuri kwenye App hiyo ya Boomplay na ni mara ya pili kwa tuzo hizo kutolewa hapa nchini.

Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli alisema, "Wasanii kama Diamond Platnumz, Alikiba, Harmonize, Rayvanny, Nandy, Mbosso, Zuchu, Aslay na Darassa ni baadhi ambao wameendelea kuvunja rekodi kupitia App ya Boomplay na ni furaha yetu kuwatambua na kuwapa tuzo.

Stambuli alisema pamoja na mambo mengine ambayo wameendelea kushirikiana na wasanii, huu ni uthibitisho wa dhamira yao ya kuendelea ya kuhakikisha tasnia ya muziki inaendelea kukua na kusonga mbele.

"Kama Kampuni inayoongoza kwenye utoaji wa huduma ya kusikiliza na kupakua muziki Afrika, Boomplay siku zote ipo mstari wa mbele katika kutambua wasanii wanaoendelea kufanya vizuri kwa kuvunja rekodi mbalimbali kupitia kazi zao za muziki. Matarajio ya Kampuni ni kuona wasanii wengi zaidi wanapata tuzo hizi kila mwaka," alisema Stambuli.

Michezo
Jumatano Julai 14, 2021
Nipashe



Solskajaer ajitokeza kumtuliza Rashford

HABARI UK. 22



Wahezaji wa Timu ya Simba Queens, wakishangilia na kombe lao baada ya kukabidhiwa kwa kuwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# GOMES AFUNGUKA WATACHEKA KIGOMA

●●●Dalali naye atangaza kuongeza nguvu kwenye kikosi cha Mnyama ili kujibu mapigo ya...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, amesema anaendelea kukiimarisha kikosi chake kwa sababu anafahamu bado hawajamaliza kazi na wana deni la kuhakikisha wanatetea ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA ambao wanaushikilia.

Simba maarufu Wekundu wa Msimbazi ambao ni mabingwa watetezi wa mashindano hayo watakutana na watani zao Yanga katika fainali ya michuano hiyo itakayochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gomes alisema lengo la kikosi chake msimu huu lilikuwa ni kufanya vyema katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Bara na kibarua kilichobakia ni kutwaa ubingwa wa FA.

Gomes alisema anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yaliyoko katika kikosi chake ili wapate matokeo mazuri ambayo yatawapa furaha zaidi wachezaji, viongozi na mashabiki wa timu hiyo.

Kocha huyo wa zamani wa El Merreikh alisema ameshafahamu uimara na mapungufu ya watani zao, hivyo watajipanga kuingia tofauti na hatimaye kutimiza malengo waliyokuwa nayo wakati wanaanza msimu huu.

"Tutaingia uwanjani tukiwa hatuna presha kwa sababu tayari tumeshachukua taji kubwa la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa kilichoko mbele yetu ni Kombe la FA, sisi ni tofauti na wenzetu ambao hawana chochote mkononi," alisema Gomes.

Aliongeza kikosi chake kitacheza soka la utulivu lakini wakiingia kwa kuwaheshimu wapinzani wao ambao wanahitaji kumaliza pia kwa ushindi ili wapate kombe msimu huu.

"Tutacheza mechi hiyo kwa malengo, itakuwa ni Simba nyingine tofauti ambayo haijawahi kuonekana msimu huu, mechi mbili za ligi tulizocheza dhidi ya KMC na Coastal Union zimetusaidia kurejea kwenye ushindani, sasa tumebakia na kazi moja ya kupambana kutetea Kombe la FA, ingawa najua haitakuwa mechi rahisi," Gomes aliongeza.

Alisema ili kuhakikisha wanafikia malengo yao, watapambana kushinda mechi mbili za ligi zilizobakia watakazocheza dhidi ya Azam na Namungo kwa sababu ya kuendelea 'kuung'arisha' ubingwa walioteta.

Naye Mwenyekiti wa zamani wa Simba, Hassan Dalali alisema jana anawataka mashabiki wa klabu hiyo kujiandaa 'kucheka' kwa sababu timu yao itapata ushindi katika mchezo huo unaosubiriwa huko Kigoma.

Dalali alisema kwanza anajivunia kikosi imara ambacho timu hiyo inacho, lakini amejipanga kudhibiti 'michezo michafu' yote kuelekea mtanange huo.

"Mimi nitakuwapo Kigoma, nasema kila linapokuwapo kombe mbele yetu na tunacheza na Yanga, basi ujue sisi lazima tutashinda, naomba msubiri kuona kitakachotokea huko," alitamba Dalali.

Kiongozi huyo amelazimika kutoa kauli hiyo huku akimbeza Mzee Mpili ambaye ametamba hivi karibuni kwamba alichangia ushindi wa timu yake ya Yanga.

Simba ilitinga fainali za Kombe la FA kwa kuwafunga Azam FC wakati Yanga yenyewe ilitangulia hatua hiyo kwa kuwaondoka Biashara United ya Musoma mkoani Mara.

## Yanga yamwandalia sherehe Niyonzima

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga inatarajia kumuaga kiungo wake wa kimataifa kutoka Rwanda, Haruna Niyonzima ambaye anatarajiwa kumaliza mkataba wa kuitumikia klabu hiyo baada ya msimu huu kumalizika.

Yanga imeandaa sherehe za kumuaga mchezaji huyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati itakapokuwa inacheza mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema kesho itakuwa ni siku maalum kwa ajili ya Niyonzima ambaye ameitumikia klabu hiyo kwa mafanikio na muda mrefu kuliko klabu nyingine ya Simba ambayo aliwahi kuitumikia hapa nchini.

"Kwanza ni heshima, pia tunafanya hivyo kwa sababu ya kutambua mchango wake kwenye klabu yetu ya Yanga. Sisi ni waungwana kwa hiyo ni lazima tumuage kwa kumfanyia sherehe, hatuko kama baadhi ya klabu ambazo zikitaka kuwaacha wachezaji wao lazima wagombane, wampe jina baya, sijui watake kumpeleka wapi, hapana. Tunataka dunia nzima itutambue kuwa Yanga ni waungwana," alisema Bumbuli.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuja kwa wingi na kujumuika kwa ajili ya kumuaga mchezaji huyo, lakini kuna kitu kikubwa ambacho watakifanya, ingawa hakutaka kukibainisha.

"Hii itakuwa pia ni mechi ya mwisho ya Ligi Kuu msimu huu kwa Jiji la Dar es Salaam, kwa hiyo tunataka pia kuwapa shukurani mashabiki wetu. Ukweli ni kwamba itakuwa siku maalum sana na uzuri ni kwamba mechi inaanza saa 10:00 jioni ili baada ya mchezo kuna matukio mengi yatafanyika na yatakuwa ya kufana kwa faida ya wanachama, mashabiki wa klabu ya Yanga kwa ujumla," Bumbuli aliongeza.

Niyonzima ambaye alijiunga na Yanga kwa mara ya kwanza mwaka 2011 akitokea APR ya Rwanda anaondoka klabuni hapo akiwa ameichezea kwa miaka tisa, kwa vipindi viwili tofauti.

Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Rwanda (Amavubi), aliichezea Simba kwa miaka miwili kuanzia 2017 hadi 2019.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >